**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

Finance and Accounts | Public Finance Management

1980

# Maoni ya Hazina Kuhusu Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali ya Tanzania kwa Mwaka 1980

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/741

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# Maoni ya Hazina kuhusu Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali ya Tanzania kwa Mwaka 1980/81

1984
KIMEPIGWA CHAPA NA MPIGACHAPA WA SERIKALI,
DAR ES SALAAM—TANZANIA
*Bei: Sh. 14/00*

# Maoni ya Hazina kuhusu Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali ya Tanzania kwa Mwaka 1980/81

13. *Mikopo kutoka Nchi za Nje—Aya ya 24:—*

Hatua mbali mbali za kurekebisha hali zimekwishachukuliwa na HAZINA kuimarisha uhasibu wa fedha za mikopo hiyo. Matokeo yaangaliwe katika hesabu za miaka ijayo.

14. *Mikopo iliyotolewa na Hazina—Aya ya 25:—*

(a) na (b): Hakuna maoni zaidi.

(c) Ushauri wa kamati ulizingatiwa.

15. (a) *Orodha ya Hesabu ya Vitegauchumi chini ya Treasury Registrar—Aya ya 26:—*

(i)—(iv): Hakuna maoni zaidi.

(v) Hatua zimechukuliwa. Matokeo yaangaliwe katika hesabu za miaka ijayo.

(b) *Utovu katika kusimamia Mashirika Juu ya Majaribio kifedha:* Uchunguzi kuhusu suala hili bado unafanywa.

16. *Mifuko ya Maendeleo—Aya ya 27:—*

(iii) na (iv): Masuala haya bado yanafuatiliwa.

17. *Maduhuli ya Serikali—Aya ya 28:—*

(a) Suala hili bado linashughulikiwa.

(b) (i)—(iv): Hakuna maoni zaidi.

(c) Hakuna maoni zaidi.

(d) UKAGUZI ilionyeshwa kibali hicho.

## IDARA YA FORODHA

18. *Maduhuli ya Forodha—Aya ya 29:—*

(b) Ukusanyaji wa bakaa unaendelea. Matokeo yaangaliwe katika hesabu za mwaka 1982/83.

(c) Agizo la Kamati lilizingatiwa.

(d) Maelezo yalitayarishwa na kuwasilishwa UKAGUZI.

19. *Matokeo ya Ukaguzi—Aya ya 30:—*

(a) *Masuali ya Ukaguzi:*

Bidii za kuyajibu maswali hayo zinaendelea. Maendeleo yaangaliwe katika hesabu za mwaka 1982/83.

(b) *Kurejeshwa kwa ushuru uliopokelewa pungufu:*

Juhudi zinaendelea. Matokeo yaangaliwe katika hesabu za mwaka 1982/83.

20. *Potevu za Maduhuli—Aya ya 31:—*

(a) *Dar es Salaam Long Room—Sh. 887,404/15:*

Hatua za kudai bakaa hiyo zinafuatiliwa.

(b) *Customs House Arusha—Sh. 208,568/70:*

Onyo la Kamati lilizingatiwa.

21. *Ships Manifests—Wizi wa Sh. 2.11 milioni—Aya ya 32:—*

Forodha imejitahidi kuchukua hatua za kurekebisha hali Maendeleo yaangaliwe katika hesabu za miaka ijayo.

22. *Customs Entries Zimepotea—Aya ya 33:—*

Ushauri wa Kamati ulizingatiwa.

23. *Bidhaa Iliyoteremsha Pungufu—Aya ya 34:—*

(i) Uchunguzi kuhusu suala hili bado unaendelea.

(ii) Hali ni kama ya (i) juu.

(iii) Ushauri wa Kamati umezingatiwa.

24. *Uuzwaji Bidhaa Kwenye Ghala ya Forodha Usio Haki (Dar es Salaam)—Aya ya 35:—*

(a) (i): Hakuna maoni zaidi.

(ii)—(vii): Idara haijathibitisha kama ilikwishaitosheleza UKAGUZI kuhusu masuala haya.

(b), (c) na (d): Maagizo ya Kamati yalizingatiwa.

25. *Kodi ya Forodha na ya Mauzo Imetozwa Pungufu—Aya ya 36:—*

Juhudi za kujibu hoja hizo zinaendelea. Maendeleo ya ujibuji yaangaliwe katika hesabu za 1982/83.

26. *Uagizaji wa Mashine, Magari, n.k. Bila Kulipiwa Ushuru (Makontrakta wa Serikali)—Aya ya 39:—*

Uchunguzi wa suala hili bado unafanywa.

27. *Jukumu la Kupokelewa Ushuru wa Forodha juu ya Bidhaa Inayoagizwa na Kampuni za Watu Binafsi na Baadaye Kuuziwa Serikali—Aya ya 40:—*

Suala hili bado linashughulikiwa.

28. *Uthamini Bei wa Video Sets, Radio, n.k. Zilizoletwa na Wasafiri—Aya ya 41:—*

Ushauri wa Kamati ulizingatiwa.

29. *Bidhaa Inayoingia Kupitia Mpakani Namanga—Aya ya 42:—*

Hatua za kuimarisha utaratibu wa kushughulikia bidhaa za jinsi hiyo zinachukuliwa. Matokeo yaangaliwe kwenye hesabu za miaka ijayo.

30. *Transit and Other Losses of Petroleum Products—Aya ya 43:—*

(a) Juhudi za kufuatilia madai ya bakaa hiyo zinaendelea. Matokeo yaangaliwe katika hesabu za miaka ijayo.

(b) *Liquid Petroleum Gas:—*
Hakuna maoni zaidi.

31. *Bidhaa Inayosafirishwa (Exports)—Aya ya 44:—*

(a) *Bidhaa Inayosafirishwa Bila ya C.D. 3 (Forms) Declaration:*

Maendeleo ya makusanyo ya maduhuli hayo yaangaliwe katika hesabu za miaka ijayo.

## IDARA YA KODI YA MAPATO

**32.** *Maduhuli kwa Kodi ya Mapato—Aya ya 45:—*

(a) *Orodha ya Hesabu ya Maduhuli:*

(1)—(5) Ushauri wa Kamati ulizingatiwa.

(c) *Majibu ya Maswali ya Ukaguzi:*

Agizo la Kamati lilizingatiwa. Maendeleo ya Ujibuji wa maswali yanayohusika yaangaliwe kwenye hesabu za miaka ijayo.

**33.** *Mapato Yanayohusika Kutozwa Kodi Hayakutozwa—Aya ya 46:—*

Maoni ni kama kwenye 32 (c) juu.

**34.** *Short Assessment of Income Due to Incorrect Deduction—Aya ya 47:—*

Bidii za kukusanya kodi hiyo zinaendelea. Matokeo yaangaliwe kwenye hesabu za miaka ijayo.

**35.** *Kusamehewa kwa Kodi ya Meli Kunaendelea—Aya ya 48:—*

Hali ni kama ya aya 34 juu.

**36.** *Incorrect Deduction for Management Fees etc. Not actually Payable to Non-Residents—Aya ya 49:—*

Ujibuji wa hoja zinazohusika bado unaendelea.

**37.** *Short Levy of Tax Due to Adoption of incorrect Residential—Aya ya 50:—*

Juhudi za kufuatilia madai ya kodi inayohusika zinaendelea.

**38.** *Incorrect Application of Consession in Law—Aya ya 51:—*

Hatua za kukusanya fedha hizo bado zinaendelea.

**39.** *Kukosa Kupokea "Withholding Tax" Juu ya Ada Zilizolipwa kwa (Wasioishi Nchini)—Aya ya 52:—*

Suala hili bado linafuatiliwa.

**40.** *Kodi Aina P.A.Y.E. Inayopokelewa Kutokana na Mishahara ya Watumishi. Dhibiti yake ina Dosari—Aya ya 55:—*

Ushauri wa Kamati ulizingatiwa.

## KODI YA MAUZO NA MAPATO MENGINE

**41.** *Kodi ya Mauzo—Aya ya 56:—*

(a) *Kukwepa Kulipa Kodi:—*

(i) Agizo la Kamati lilizingatiwa.

(iii) Uamuzi wa Waziri wa Sheria bado unafuatiliwa.

(iv) Nyaraka ziliwasilishwa UKAGUZI.

(b) *Kutokuwasilisha Kodi Iliyotozwa:—*

Agizo la Kamati lilizingatiwa.

(c) *Tozo:*

Hali ni kama kwenye (b) juu.

(d) *Kutokukadiria Kodi:*

Mawasiliano bado yanafanywa kupata makubaliano ya tafsiri sahihi ya sheria.

42. *Kodi ya Kiwanja Pamoja na Huduma—Aya ya 57:—*

(i) Suala hili bado linashughulikiwa.

(ii) Hali ni kama ya (i) juu.

(iii) Hali ni kama ya (i) na (ii) juu.

43. *Kodi ya Starehe (Internal Revenue Office Dar es Salaam)—Aya ya 58:—*

(a) Uchunguzi bado unafanywa.

(b) (i) Suala hili bado linashughulikiwa.

44. *Training Levy—Aya ya 59:—*

(i)—(v): Masuala hayo bado yanafuatiliwa.

45. *Kodi ya Mafuta ya Petroli—Aya ya 60:—*

(a) *Fuel Ration Cards:*

Hakuna maoni zaidi.

(b) *Leseni za Shule za Kuendesha Magari:*

Hakuna maoni zaidi.

## FUNGU 34—WIZARA YA MAMBO YA NJE

46. *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 61:—*

Wizara bado haijatoa taarifa ya utekelezaji wa agizo hili la Kamati. Hata hivyo, Kamati ilizitambua bidii za Wizara za kujibu maswali ya Ukaguzi hasa maswali ya 1980/81 kwani lilisalia swali moja tu lisilojibiwa. Maendeleo ya ujibuji wa maswali yaangaliwe kwenye taarifa ya mwaka ujao.

47. *Orodha ya Hesabu ya Mali na Dhima—Aya ya 62:—*

(a) Deposits—Sh. 22,013,778/15:

Hakuna maoni zaidi.

(b) Fedha ya Amana Imetolewa Ziada—Sh. 4,462,588/75:

Mchanganuo ulitayarishwa na kutolewa UKAGUZI. Tatizo la kutolipwa kwa madeni ya zamani bado halijapatiwa ufumbuzi.

(c) Wizi wa Fedha Sh. 93,700/60 na sio Sh. 93,619/95:

Kesi bado inachunguzwa na Polisi.

48. *Masurufu na Karadha—Aya ya 63:—*

(a) Karadha za Mishahara—Sh. 1,133,930/80:

Maendeleo ya urejeshaji wa karadha za mishahara yaangaliwe kwenye taarifa ya mwaka ujao.

(b) Masurufu—Sh. 5,095,683/80:

Maoni ni kama kwenye (a) juu.

49. *Balozi za Tanzania—Aya ya 64:—*

(a) Ubalozi wa London:

(i) Maendeleo ya urejeshaji wa fedha hii yaangaliwe kwenye taarifa ya mwaka ujao.

(ii) Hakuna hoja zaidi.

(iii) Hakuna Hoja zaidi.

(iv) Marejesho yanafuatiliwa na NGOME. Hali halisi itaangaliwa kwenye hesabu za NGOME za 1981/82.

(v) Hakuna maoni zaidi.

(b) *Ubalozi wa Rome:—*

Maendeleo ya marejesho yaangaliwe kwenye hesabu za mwaka ujao.

(c) *Ubalozi wa Luanda.:—*

Maendeleo ya marejesho ya fedha iliyosalia yaangaliwe kwenye hesabu za mwaka ujao.

(d) *Ubalozi wa Lusaka:—*

Hakuna maoni zaidi.

(e) *Ubalozi wa Bujumbura:—*

(i) na (ii): Hakuna maoni zaidi.

(iii) Maendeleo ya urejeshaji wa fedha hiyo yaangaliwe katika hesabu za mwaka ujao.

(f) *Ubalozi wa Kigali:—*

(i) (1) na (2): Hakuna maoni zaidi.

(3) Maendeleo ya marejesho yaangaliwe kwenye hesabu za mwaka ujao.

(ii) (1): Hakuna maoni zaidi.

(2): Hakuna maoni zaidi.

(4): Wizara haijatoa taarifa zaidi juu ya suala hili.

(5)—(7): Hakuna maoni zaidi.

## FUNGU 37.—OFISI YA WAZIRI MKUU

50. *Masuali ya Ukaguzi—Aya ya 65:—*

Katika masuali 94 yaliyosalia tangu 1974/75 hadi 1980/81, masuali 48 yalijibiwa na 46 bado yanashughulikiwa. Maendeleo ya ujibuji yatazamwe katika hesabu za 1981/82.

51. *Malipo Yasiyo ya Kawaida au Yenye Shaka—Sh. 3,595,250/:—Aya ya 66:—*

(ii) *D.D.D.'s kwa nyumba za V.M.T.P.—Sh. 797,250/-:*

Hesabu ya matumizi iliyokwishawasilishwa ni Sh. 464,192/60. Matumizi ya Sh. 333,057/40 bado yanafuatiliwa.

(iii) *R.D.D. Kilimanjaro Operation Vijiji—Sh. 150,000/-:*

Ukaguzi waliridhika na matumizi hayo na hoja ilifungwa.

(iv) *Principal I.R.D.P. Morogoro—Sh. 2,614,000/-:*

Ofisi ya Waziri Mkuu inasubiri kupata Taarifa ya Shirika la Ukaguzi (Tanzania Audit Corporation) ndipo iweze kuhakiki matumizi ya fedha hizo.

52. *Masurufu na Karadha—Aya ya 67:—*

(a) *Kutokana na Hesabu ya Kawaida:*

Ofisi ya Waziri Mkuu haikutoa mchanganuo kuthibitisha jitihada zinazofanywa katika kudai marejesho ya karadha na masurufu hayo Karadha za Binafsi Sh. 13,202/-, Karadha zingine Sh. 1,439,367/05 na (Masurufu Sh. 435,420/70). Maendeleo ya urejeshaji yatazamwe katika hesabu za 1981/82.

(b) *Kutokana na Hesabu ya Maendeleo—Sh. 169,277/20:*

Mchanganuo wa matumizi ya hesabu hii haukutolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu ingawa ilijibu kuwa imeutayarisha.

53. *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka na Yenye Hati Pungufu—Aya ya 68:—*

Nyaraka zenye thamani ya Sh. 43,244,210/40 (matumizi yasiyo na nyaraka) na zingine za Sh. 2,097,321/05 (matumizi yenye hati pungufu) zilipatikana, na hoja zinazohusika zilijibiwa na kufungwa. Nyaraka za Sh. 903,106/80 zenye hati pungufu bado zinashughulikiwa.

54. *Hesabu ya Maendeleo—Aya ya 69:—*

(a) U.W.T.—Sh. 560,000/-.

(b) Kilombero Rural Roads Maintenance—Sh. 5,000,000/-.

(c) Town Engineering kwa Mikoa—Sh. 910,000/-.

(d) Chuo cha Ushirika Moshi—Sh. 14,168,000/-.

(e) Tech. Asst. Rural Roads Maintenance—Sh. 2,576,000/-.

Pamoja na kueleza kwamba Ukaguzi walishiriki katika safari ya kuona baadhi ya miradi, Ofisi ya Waziri Mkuu haijathibitisha kama imewasilisha maelezo ya kuitosheleza Ukaguzi juu ya mada hii.

55. *Matumizi Yaliyofanyika Hayapo Kwenye Makadirio ya—Sh. 1,137,109/85—Aya ya 70:—*

Suala hili bado linashughulikiwa kati ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Hazina.

56. *Usuluhisho wa Hesabu ya Benki na Shahada ya Usahihi—Aya ya 71:* —Hazina bado inalishughulikia suala hili.

## FUNGU 38—WIZARA YA ULINZI (NGOME)

57. *Hesabu za Jumla na Orodha Zake, 1980/81—Aya ya 72:—*

Afisa Mhasibu alizingatia agizo la Kamati na kuahidi kurekebisha hali miaka ijayo.

58. *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 73:—*

NGOME haikuweza kuyajibu maswali yote kama ilivyoagizwa na Kamati. Bidii za kujibu zinaendelea na maswali 386 yamekwishajibiwa. Maendeleo yaangaliwe kwenye hesabu za mwaka 1981/82.

59. *Karadha Zinazodaiwa na Masurufu—Aya ya 74:—*

(a) *Karadha za Binafsi—Sh. 9,322,615/35:—*

(i) Mchanganuo ulitayarishwa na kuwasilishwa UKAGUZI.

(b) *Masurufu—Sh. 42,167,318/45:—*

Mchanganuo ulitayarishwa na kuwasilishwa UKAGUZI.

60. *Matumizi Yenye Hati Pungufu—Sh. 6,524,309/65—Aya ya 75:—*

Maswali ya ukaguzi manne ya Sh. 282,003/- yamejibiwa na kufungwa. Maswali mengine bado yanashughulikiwa. Maendeleo ya ujibuji wa maswali hayo yaangaliwe kwenye hesabu za 1981/82.

61. *Malipo Yasiyo Kawaida na/au Yenye Shaka—Aya ya 76:—*

(a) *Malipo kwa Ankara Vifani—Sh. 4,487,030/70:*

Maswali manne ya Sh. 2,101,422/90 yamefungwa. Mengine bado yanashughulikiwa.

(b) *Malipo Yaliyofanyika kwa Nyaraka Zinazotuhumiwa kuwa za Kubuniwa—Sh. 737,072/:*

Matokeo ya uchunguzi wa Polisi ya Jeshi (Military Police) bado hayajatolewa na NGOME. Hata hivyo swali moja Sh. 191,992/- limekwishafungwa.

(d) *Malipo kwa Ziada—Sh. 67,566/25:—*

Ni swali la ukaguzi moja tu la Sh. 4,200/- lililothibitishwa kufungwa. Mswali mengine bado yanafuatiliwa.

(e) *Gharama za Bima—Sh. 360,000/—*

Baada ya maelezo ya NEDCO kwenye mkutano wa Kamati wa tarehe 17 Januari, 1983, ilifahamika kwamba gharama za bima ni sehemu ya kiasi cha mkataba (contract sum) na hurejeshwa kwa mjenzi kama gharama nyingine. UKAGUZI iliyakubali maelezo hayo hivyo kuondoa haja ya kutafuta ushauri wa Mwanasheria Mkuu.

62. *Utovu wa Dhibiti Katika Ulipaji wa Mishahara, Posho n.k.—Aya ya 77:—*

(a) *Malipo Maradufu:*

(b) *Malipo ya Posho kwa Ziada—Sh. 36,101,60:*

Matokeo ya uchunguzi kuhusu nyaraka za (a) bado hayajatolewa na NGOME. Hoja tatu zinazohusika zimepatiwa majibu ambayo yamewasilishwa UKAGUZI.

(c) *Malipo ya Mishahara kutoauniwa na Hati Zilizotiwa Stakabadhi za Walipwa*— (*Sh. [illegible]3/65*):

Maendeleo ya ujibuji wa maswali yanayohusika yaangaliwe katika hesabu za 1981/82.

(d) *Malipo Yanayotuhumiwa kuwa ni ya Wizi*—(*Sh. 1,923,865/-*):

Matokeo ya upelelezi wa Polisi bado hayajapatikana.

(e) *Karadha za Mishahara kulipwa Visivyo Kawaida*—(*Sh. 33,000/-*):

Hali ni kama (d) juu.

63. *Tuhuma ya Wizi—Aya ya 80:—*

(a) *School of Artillery, Arusha*—(*Sh. 1,729,897/30*):

Matokeo ya kesi bado hayajapatikana.

(b) 303 *KJ Arusha*—(*Sh. 112,027/25*):

Maendeleo ya marejesho yaangaliwe katika hesabu za mwaka 1981/82.

64. *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 81:—*

NGOME ilizingatia agizo la Kamati. Mwelekeo mpya utazamwe katika hesabu za miaka ijayo.

## FUNGU 39—JESHI LA KUJENGA TAIFA

65. *Masuali ya Ukaguzi—Aya ya 82:—*

Wizara ilishindwa kutekeleza kikamilifu agizo la Kamati na kwa kweli hata bidii za kulitekeleza agizo hilo hazikuonekana. Hadi sasa (wakati wa kuandika Maoni haya) ni maswali 26 tu yalikwishajibiwa kati ya yote 211 yaliyokuwa yamesalia wakati wa Kikao cha Kamati. HAZINA imehimiza Afisa Mhasibu kuongeza juhudi katika kuyashughulikia maswali hayo.

66. *Masurufu na Karadha—Aya ya 84:—*

Afisa anayehusika na wenzake alioshirikiana nao katika wizi ambao ulifikia kiasi cha Sh. 190,250/- walishtakiwa na kufungwa miaka 6 kila mmoja. Kazi ya kurekebisha usuluhisho wa hesabu bado inafanywa. Maendeleo ni madogo kutokana na hesabu hizo kuvurugwa sana makusudi

67. *Usuluhisho wa Hesabu za Benki na Shahada ya Usahihi—Aya ya 85:—*

Usuluhisho wa hesabu za Benki kwa akaunti zote ulikwishakamilishwa hadi tarehe 30 Juni, 1981 na kuwasilisha UKAGUZI.

68. *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka na Yenye Nyaraka Pungufu—(Sh. 36,494,181/50)—Aya ya 86:—*

Wizara ilithibitisha kupatikana kwa nyaraka kama ifuatavyo:—

| | | | |
|---|---|---|---|
| (i) | Matumizi Yasiyo kuwa na Nyaraka ... ... | 28,642,424 | 10 |
| (ii) | Matumizi Yenye Hati Pungufu ... ... | 1,153,915 | 85 |
| (iii) | Malipo ya S.D.U. ... ... ... ... ... | 90,903 | 85 |
| | Jumla ... | 29,887,243 | 80 |



2

(b) *Masurufu va Safari—(Sh. 242,668/45):*

Wizara imetoa taarifa kwamba Sh. 158,738/45 zimekwisharejeshwa na Sh. 83,930/- zilizobaki bado zinakatwa kwenye mishahara ya wahusika. Maendeleo ya urejeshaji wa fedha hiyo yataangaliwa katika hesabu za mwaka ujao.

(c) *Karadha za Mishahara—(Sh. 54,264/20):*

Vilevile Wizara imetoa taarifa kwamba Sh. 51,331/70 zimekwisharejeshwa na kwamba Sh. 2,932.50 zilizosalia zinakatwa kwenye mishahara ya wadaiwa. Maendeleo yataangaliwa katika hesabu za mwaka ujao.

**69.** *Ulegevu Katika Dhibiti ya Nunuzi na Utoaji Hesabu ya Vifaa—Aya ya 87:—*

(a) *Malipo kwa kutolewa Ankra Vifaa—(Sh. 2,802,882/10):*

Kwanza Wizara ilithibitisha kwamba vifaa vinavyohusika ni vya thamani ya Sh. 4,803,298.60 na siyo Sh. 2,802,882.10 kama ilivyohojiwa. Pili taarifa ya Wizara ilithibitisha kwamba vifaa vya Sh. 622,409/- tu bado vinatafutiwa kumbukumbu za mapokezi.

(b) *Bidhaa iliyolipwa haikupokelewa au Kupokelewa Pungufu—(Sh. 733,829/30):*

(i) *Mafuta ya kupikia—(Sh. 145,400/-):*

Madebe 115 ya mafuta ya kupikia yenye thamani ya Sh. 101,749/- yalithibitishwa kupokelewa. Mwuzaji alishindwa kutoa madebe 45 na alirejesha thamani ya Sh. 32,715/-. Madebe 40 yenye thamani ya Sh. 10,936/- hayakupokelewa ijapokuwa yalionyeshwa vitabuni kuwa yalipokelewa. Afisa Mhasibu aliamua kumtoza kiasi hicho afisa anayehusika na makato yanaendelea.

(ii) *Nyuzi za Kushonea—(Sh. 113,490/-):*

Wizara bado inafanya bidii za kumtafuta mfanyabiashara anayehusika ili achukuliwe hatua za kisheria.

(iii) *Nyama—(Sh. 18,200/-):*

Sh. 3,000/- zilikwisharejeshwa na mhusika. Sh. 15,200/- bado hazijarejeshwa kwa kuwa mhusika yungali kizuizini. Hatua za marejesho zitachukuliwa mara tu akitoka kizuizini.

(iv) *Sarugi—(Sh. 11,787/50):*

Hakuna maoni zaidi.

(v) *Hard Board Sheets—(Sh. 153,281/80):*

Wizara imetoa taarifa kwamba kati ya "Hard Board Sheets" 200 zenye thamani ya Sh. 9,320/-, 133 zilipokelewa na kuingizwa kwenye Madaftari ya Vifaa. Taarifa hiyo imeeleza pia kwamba tofauti ya "Hard Board Sheets" 73 ilisababishwa na kupanda kwa bei kutoka Sh. 46.60 kufikia Sh. 70.85.

(c) *Pungufu za Vifaa:*

(i) *Mablanketi:*

Wizara iliamua kuhesabu thamani ya mablanketi hayo ya Sh. 3,900/- kama hasara ya Serikali. Afisa anayehusika ametakiwa ajitetee kwa nini asitozwe fedha hiyo.

(ii) Kitambaa cha aina Cotton Drill Grey Mita 5,545:—

Upotevu huu bado unafuatiliwa.

(iii) Kitambaa cha Mashuka Mita 1,285:—

Afisa anayehusika ametakiwa kutoa taarifa ya upotevu huu kusudi wafahamike wengine wanaohusika na kuchukuliwa hatua zinazostahili.

(iv) Mchele Kg. 950:

Uthibitisho wa kutopotea kwa mchele huo ulitolewa kwa UKAGUZI.

**70.** *Ulegevu katika Ukusanyaji na Uwekaji Hesabu ya Maduhuli ya Mauzo—Aya ya 88:—*

(a) *Fedha ya Mauzo Isiyowasilishwa Benki (Sh. 63,245/-):—*

Suala hili bado linafuatiliwa.

(b) *Madai Sh. 889,283.20:—*

Uchambuzi wa madeni hayo bado unafanywa ili Wizara/Idara zinazodaiwa ziweze kufuatwa na kulipishwa.

(c) *Fedha ya Mauzo Haimo Hesabuni—Sh. 30,746/50:—*

Wizara ilitekeleza maagizo ya Kamati.

**71.** (a) *Utolewaji Ziada ya Sukari Sh. 19,157.50—Aya ya 89:—*

UKAGUZI ilipatiwa uthibitisho wa maelezo kuhusu upungufu huo wa Sukari.

(b) *Upungufu wa Vitu Boharini—Sh. 25,691.90:—*

Hatua za kuhalalisha upotevu huu bado hazijakamilishwa na Wizara.

**72.** *Malipo Yanayotia Shaka—Sh. 119,765.20—Aya ya 90:—*

Hakuna maoni zaidi.

**73.** *Ununuzi wa Ng'ombe Usio wa Busara (Sh. 313,900/-)—Aya ya 91:—*

Hatua za kuhalalisha ununuzi huo bado hazijakamilishwa na Wizara.

**74.** *Ukodishaji wa Magari (Sh. 269,827.50)—Aya ya 92:—*

Wizara ilikwishachukua hatua za kuomba uhalalisho wa malipo hayo.

**75.** (ii) *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 93:—*

(a) *Upotevu wa Vifaa MMJKT (Sh. 24,721.80):—*

Sasa umewekwa utaratibu wa kuhakikisha kuwa taarifa za Uhakikimali zinajibiwa mara moja.

(b) *Upotevu wa Ng'ombe JKT Lugalo (Sh. 13,200/-):—*

Mhusika mmoja ambaye angekatwa Sh. 2,000/- alitoroka Jeshini na bado anatafutwa. Mhusika mwingine anakatwa fidia ya Sh. 4,600/-.

(c) *Upotevu wa Pikipiki JKT Mgulani (Sh. 8,776/-):—*

Imeamuliwa afisa aliyesababisha hasara hiyo atozwe thamani ya pikipiki hiyo.

(d) *Upotevu wa Mafuta ya Nazi JKT Mgulani (Sh. 10,000/-)—*

Wahusika wanatafutwa baada ya kutumikia kifungo ili watozwe fidia.

(e) *Upotevu wa Shuka 160—JKT Mgulani (Sh. 12,328/-):—*

Maafisa wawili wanakatwa jumla ya Sh. 8,209.70.

76. *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 94:—*

Hali ya sasa ni kuwa yamesalia maswali 306 yasiyojibiwa ya miaka 1977/78 hadi 1980/81. Idara ilikwishaunda kikosi cha kushughulikia maswali hayo. Maendeleo yatazamwe katika hesabu za mwaka ujao.

77. *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka na Yenye Hati Pungufu—Sh. 520,307.80—Aya ya 96:—*

Nyaraka zenye thamani ya Sh. 73,365.15 zimepatikana; kwa hiyo kiasi; cha Sh. 228,044.50 (malipo yenye hati pungufu Sh. 150,137.50 na malipo ya posho bila kustakabadhiwa Sh. 77,907/-) bado hakijapatiwa nyaraka/hati.

78. *Malipo Yenye Shaka—Aya ya 97:—*

(a) Hati ya umilikaji wa jengo la Mahakama Kuu Mbeya bado haijatolewa kwa Idara. Hatua za kulifuatilia suala hilo zinaendelea.

(b) *Malipo ya Karadha Yamehesabika moja kwa moja kuwa ni Gharama—Sh. 819,735.75:—*

Nyaraka zenye thamani ya Sh. 184,860.05 zilikwishapatikana na kusalia hati zenye thamani ya Sh. 591,325.70 kama ifuatavyo:—

| | Sh. |
|---|---|
| Kazi ndogo ndogo ... ... ... | 581,225.70 |
| Ununuzi wa Vifaa/huduma ... ... | 9,000.00 |
| Kulipia posho ... ... ... ... | 1,100.00 |
| | 591,325.70 |

(c) *Hati za Ukamilishaji wa Kazi Hazikupokelewa—Sh. 340,621.10:—* Hati za ukamilishaji wa kazi zenye thamani ya Sh. 53,232.50 zimepatikana. Bado hati zenye thamani ya Sh. 198,827.15.

79. (a) *Malipo kwa Ankra Vifani Sh. 304,461.35—Aya ya 98:—*

Hoja 5 zenye thamani ya Sh. 20,366/- zimejibiwa. Hoja 17 zenye thamani ya Sh. 51,871.75 bado zinashughulikiwa.

(b) *Vifaa Havikuwekwa Kwenye Hesabu—Sh.264,396/-:—*

Hoja 11 zenye thamani ya Sh. 71,786.15 zimejibiwa. Zimesalia hoja 27 zenye thamani ya Sh. 120,464.65.

80. (a) *Malipo Ziada kwa Wauzaji—Sh. 67,465.95—Aya ya 99:—*

Hatua za kuhalalisha malipo hayo zinaendelea. Hadi sasa kiasi kilichohalalishwa ni Sh. 5,579.05 tu.

(b) *Malipo kwa Masurufu Sh. 36,000/-:—*

Idara haikuweza kutoa uthibitisho wowote kuhusu kufidiwa kwa malipo hayo. Ila Idara imesisitiza kwamba haikulipa kodi ya nyumba kwa mwaka mzima wa 1980 ambayo ilichukuliawa kama fidia ya malipo hayo.

**81.** *Utengenezaji wa Huduma ya magari Kwenye Gereji za Watu Binafsi Wasiopewa Zabuni Sh. 1,113,176.95—Aya ya 100:—*

Hoja 15 zenye thamani ya Sh. 242,478.45 zimejibiwa. Hoja zenye thamani ya Sh. 522,155.45 bado zinafuatiliwa.

**82.** *Utovu wa Dhibiti Katika Ukusanyaji wa Maduhuli na Uwekaji Hesabu wa Amana Zinazopokelewa—Aya ya 101:—*

(i) *District Court Kilosa—Sh. 93,321.55:—*

Taarifa ya upotevu ilikwishatayarishwa. Mtuhumiwa amekwisha-hukumiwa. Idara haijapokea nakala ya hukumu.

(ii) *Kariakoo Primary Court Dar es Salaam Sh. 1,562.95 na Sh. 6,071/-:—*

Mtuhumiwa aliachiliwa na Polisi. Idara imeamua kumtoza Karani anayehusika kiasi chote cha hasara kwa makato ya Sh. 200/- kila mwezi kuanzia mwezi Machi, 1984.

(iii) *Temeke Primary Court Dar es Salaam—Sh. 70,209.65 na Sh. 176/-; Sh. 49,135.70 na Sh. 49,199.60:—*

Idara bado inalifuatilia suala hili.

**83.** (a) *Potevu za fedha Taslim—Sh. 170,785.35—Aya ya 102:—*

(b) *District Court Kigoma—Sh. 70,723.15:—*

Kesi zihusuzo wizi huu bado ziko Mahakamani.

## FUNGU 42—OFISI YA SPIKA

**84.** *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 103:—*

Ofisi ilijitahidi sana kujibu maswali ya Ukaguzi yanayohusika na hadi tarehe 30 Juni, 1983 yalikwishajibiwa maswali 187 na kusalia maswali 191 Kati ya maswali hayo yaliyosalia, maswali 118 yanahusu Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1975 ambayo Wilaya za Uchaguzi zinazohusika zilishindwa kabisa kuyapatia majibu na OFISI inaomba kibali cha kuyafunga. HAZINA inaliunga mkono ombi hilo kwa misingi ya Aya ya 448 ya Taarifa ya Kamati.

**85.** *Masurufu kwa Shughuli za Uchaguzi Mkuu—Aya ya 104:—*

Hadi tarehe 30 Juni, 1983 masurufu ya Sh. 1,177,032/20 yalikuwa hayajarejeshwa na Wilaya mbali mbali za Uchaguzi. OFISI inaendeleza juhudi za kufuatilia.

**86.** *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka na Yenye Hati Pungufu—(Sh. 223,932/90)—Aya ya 105:—*

Maswali yanayohusika bado yanafuatiliwa kwenye Wilaya za Uchaguzi zinazohusika.

## FUNGU 43—WIZARA YA KILIMO

**88.** *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 110:—*

Wizara imekwishajibu maswali 364 kati ya yale 676 yaliyosalia wakati wa Kikao cha Kamati. Bidii za kufuatilia maswali hayo zinaendelea. Maendeleo ya ujibuji yaangaliwe katika hesabu za mwaka ujao.

89. *Matokeo ya Hesabu—Aya ya 111:—*

(a) *Hesabu ya Matumizi ya Kawaida—Bakaa Sh. 99,740/-:—*

Wizara imetoa taarifa kwamba uchunguzi ulifanywa na ilijitosheleza kwamba hakuna mtumishi aliyelipwa mishahara miwili au zaidi.

(b) *Hesabu ya Matumizi ya Maendeleo—Bakaa Sh. 28,173,112/50:—*

Wizara ilitoa mwongozo kwa maafisa wake wanaohusika kuhusu utekelezaji wa agizo la Kamati.

90. *Hali ya Uwekaji Hesabu na Shahada ya Usahihi—Aya ya 112:—*

Maendeleo ya Kazi hii ni madogo mno kwa sababu hesabu nyingine zimekwishakuwa za miaka ya zamani na upatikanaji wa nyaraka unakuwa mgumu. Wizara imeshauriwa kutilia mkazo zaidi usuluhisho wa hesabu mpya kuliko zile za zamani.

91. *Masurufu Yasiyorejeshwa—Sh. 2,507,517/30—Aya ya 113:—*

(a) Standing Imprests—Sh. 497,704/50.

(b) Masurufu ya Safari—Sh. 2,009,812/80.

Marejesho yanaendelea kufanywa kila mwezi. Maendeleo yaangaliwe katika hesabu za mwaka ujao.

92. *Masurufu na Karadha za Mishahara yameingizwa moja kwa moja Hesabu Kama ni Matumizi—Sh. 120,667/35—Aya ya 114:—*

(iii) M.A.T.I. Ilonga—Sh. 17,874/-:—

Marejesho yanaendelea kufanywa. Wakati wa kuandika Maoni haya ilisalia bakaa ya Sh. 2,000/- tu.

93. *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka na yenye Hati Pungufu—Sh. 10,546,519/40—Aya ya 115:—*

Taarifa ya Wizara ilionyesha hali ya malipo ambayo bado kuhalalishwa kama ifuatavyo:—

| | Sh. |
|---|---|
| (a) Malipo Yasiyokuwa na Nyaraka ... ... ... | 174,075/35 |
| (b) Malipo bila Kuauniwa na Nyaraka ... ... | 32,840/00 |
| (c) Malipo kwa Ankra Vifani ... ... ... ... | 1,378,519/90 |
| Jumla ... | 1,585,435/25 |

94. *Malipo ya Batili—(Sh. 729,859/55)—Aya ya 116:—*

Bidii za kushughulikia hoja zinazohusika zinaendelea. Sasa yamesalia maswali yenye thamani ya Sh. 53,330/25.

95. *Potevu za Fedha—Sh. 3,307/85—Aya ya 117:—*

Hatua za kisheria/kinidhamu dhidi ya watuhumiwa zinaendelea. Matokeo bado kupatikana.

96. *Makosa ya Kasoro Kwenye Mahesabu—Aya ya 118:—*

(a) Wizara ililizingatia onyo la Kamati.

(b) Kiasi hicho kilikwisharekebishwa na hoja inayohusika ilifungwa.

(c) Hatua ya uhasibu iliyochukuliwa ilikuwa sahihi kwa mujibu wa Kanuni za Fedha.

97. *Malipo ya Mishahara yanayotia Mashaka—Aya ya 119:—*

(a) Malipo ya Mishahara Yasiyo Sahihi—Sh. 35,520/-.

Mhusika amekwishakatwa jumla ya Sh. 3,700/- kwenye mshahara wake. Makato yanaendelea.

98. *Malipo kwa Washauri—Sh. 616,000/-—Aya ya 120:—*

(a)—(c) Hakuna maoni zaidi.

99. *Matumizi Haya Kutolewa Hesabu Hesabu yake—Aya ya 121:—*

(a) Wizara bado inawasiliana na wafadhili wanaohusika kuhusu suala hili.

100. *Hesabu ya Matumizi ya fedha ya Miradi ya Misaada—Aya ya 122:—*

(a) F.A.O. Project:

Wizara iliipatia UKAGUZI maelezo zaidi kuhusu suala hili.

## FUNGU 46.—WIZARA YA ELIMU YA TAIFA

101. *Taahira Kuleta Hesabu—Aya ya 123:—*

Hesabu za mwaka 1981/82 zimewasilishwa Ukaguzi. Wizara inaendelea kufanya jitihada ili kila mwaka iweze kuwasilisha Hesabu kwa mujibu wa Sheria. Hesabu za 1982/83 ziliwasilishwa Ukaguzi 3.11.83.

(i)—(iv): Hakuna maoni ya zaidi.

102. *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 124:—*

Wizara imejibu maswali 727 na imebakiza maswali 1944 ya tangu 1975/76 hadi 1980/81. Maendeleo ya ujibuji yatazamwe katika mwaka 1981/82.

103. *Madaftari ya Fedha Taslimu ya Hesabu ya Matumizi na Maduhuli—Aya ya 125:—*

(a) *Daftari la Fedha Taslimu (Malipo):—*

Wizara inaendelea kutoa mafunzo—kazini kwa Watumishi wake ili kupunguza makosa hayo.

(b) *Daftari la Fedha Taslimu (Maduhuli):—*

Hoja ilijibiwa kikamilifu na kufungwa.

104. *Usuluhisho wa Hesabu ya Benki na Shahada ya Usahihi—Aya ya 126:—*

(a) *Hesabu ya Matumizi ya Kawaida:—*

Usuluhisho wa Hesabu za Matumizi ya Kawaida na Amana za mwaka 1980/81 ulikamilika na kuwasilishwa Ukaguzi.

(b) *Hesabu ya Matumizi ya Maendeleo:—*

(i)—(iv): Hakuna maoni ya zaidi.

**105.** *Mambo yasiyo Kawaida katika Kutoa Masurufu na Utolewaji wa Hesabu yake—Aya ya 127:—*

(ii) *Matumizi ya Petroli—Shs. 17,653/25 na Dizeli Sh. 39,012/60:—* Wizara bado inatafuta majibu ya hoja zinazohusu matumizi hayo.

(iii) *Gharama za Kukodi (Taxi)—Sh. 44,124/60:—*

Wizara iliwasilisha Ukaguzi maelezo ya matumizi ya Shs. 9,230.80. Hoja ya Shs. 580/- iliyobakia bado inashughulikiwa.

(iv) *Risiti za Bandia—Sh. 21,507/60:—*

Majibu ya hoja inayohusu Sh. 13,408.80 yaliwasilishwa Ukaguzi. Wizara bado inashughulikia hoja iliyobakia inayohusu Sh. 8,098.80.

(v) *Manunuzi ya Petroli Sh. (34,481/60 na Dizeli Sh. 24,367/20):—*

Masuali yanayohoji ununuzi wa petroli ya Sh. 34,481.60 na dizeli ya Sh. 24,367.20 yalijibiwa na kuwasilishwa Ukaguzi.

(vi) *Gharama zilizozidi Masurufu yaliyotolewa Sh. 14,894/30:—*

Hoja mbili zenye thamani ya Sh. 7,845.80 bado zinashughulikiwa.

(vii) *Malipo Bila Kuidhinishwa na Afisa Muidhinishaji:—*

Katika zile hoja mbili zilizohusu suala hili, hoja moja ilijibiwa na kufungwa na nyingine bado inashughulikiwa.

(viii) *Kutorejeshwa Masurufu Ipasavyo—Sh. 730,323/90:—*

Wizara bado inashughulikia hoja nne zinazohusu urejeshaji wa masurufu haya.

**106.** *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka na Yenye Hati Pungufu—Sh. 8,259,138/80—Aya ya 128:—*

(a) Wizara iliwasilisha Ukaguzi nyaraka zenye thamani ya Sh. 5,287,468.80 zilizohusu matumizi yasiyokuwa na nyaraka na yenye Hati pungufu. Nyaraka za matumizi ya Sh. 2,296,912.75 bado zinashughulikiwa.

(b) Wizara bado inafanya jitihada za kupata majibu ya kupeleka Ukaguzi.

**107.** *Malipo Yasiyo Kawaida na au Yenye Shaka—Aya ya 129:—*

(a) *Malipo ya Posho ya Safari Sh. 8,000/-:—*

Hoja inayohusu malipo haya ilijibiwa na kufungwa.

(b) (i) *Malipo Zaidi kwa Wazabuni—Sh. 11,807/75:—*

(ii) *Malipo Maradufu ya Posho—Sh. 6,749/50:—*

Wizara iliwasilisha Ukaguzi majibu ya hoja zilizohusu malipo ya (ii). Hoja juu ya malipo ya (i) bado zinashughulikiwa.

(c) *Manunuzi ya Karatasi na Vitu Vingine vya Office—Sh. 154,910/-:—*

Majibu ya hoja moja iliyohusu Sh. 7,700/- yaliwasilishwa Ukaguzi. Wizara inaendelea kushughulikia hoja tano zinazohusu Sh. 147,210/-.

(d) *Potevu za Mishahara—Sh. 45,280/-:—*

(i) *Tarime Chuo cha Elimu ya Taifa—Sh. 19,488/20:—*

(ii) *Tabora Chuo cha Elimu ya Taifa—Sh. 25,791/80:—*

Watuhumiwa wameachiliwa huru na Mahakama. Wizara inawasiliana na Hazina juu ya ufutaji wa potevu hizo.

108. *Agricultural Unit—Ndanda Secondary School—Sh. 277,448/90—Aya ya 131:—*

Kontrakta M/S. DEMACCO & CO. alifikishwa Mahakamani ili kumtaka arejeshe zile Sh. 233,793/60 zilizobakia. Kesi bado inaendelea Mahakamani.

109. *Malipo ya Ulaghai/Wizi na Potevu ya Fedha—Aya ya 132:—*

(a) *Malipo ya Ulaghai—Sh. 324,426/75:—*

(b) *Wizi—Sh. 105,403/-:—*

(c) *Potevu ya Fedha—Sh. 172,778/10:—*

Wizara ilitayarisha Taarifa za Upotevu wa fedha hiyo na kuziwasilisha Hazina. Ukaguzi walijulishwa juu ya hatua hiyo iliyochukuliwa.

110. *Mwanza Literacy Project Centre—Aya ya 133:—*

(i)—(v): Wizara iliridhika kwamba Ndugu E. P. Mbakile aliyekuwa M'kurugenzi wa Kituo hicho cha Mwanza anahusika na upotevu wa Sh. 319,812/40. Pia amehusishwa na uidhinishaji wa karadha na masurufu ambayo hayajarejeshwa ya Sh. 83,619/30 na matumizi yasiyoauniwa na nyaraka ya Sh. 22,175/75. Hatua za kisheria na za kinidhamu zinachukuliwa na Wizara dhidi ya Ndugu Mbakile. Karadha na masurufu yaliyobakia yatarejeshwa kutokana na mishahara ya Watumishi wanaodaiwa malipo hayo.

111. *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 134:—*

(a) *Magamba Shule ya Secondari—Lushoto:—*

(iv) Vifaa mbali mbali—Sh. 87,425/-

Bodi Maalum ya Ukaguzi wa Vifaa vya Serikali (Special Board of Survey) ilikagua vifaa hivyo na kuwasilisha mapendekezo yake Hazina.

(v) *Vifaa vyenye thamani ya Sh. 299,269/-:—*

Hakuna maoni ya zaidi.

(b) *Mkwawa Chuo Chuo cha Elimu ya Taifa—Sh. 12,900/:—*

Wizara ilifidiwa—Sh. 1,735/- kwa vitabu vilivyopotea. Taarifa ya Upotevu ilitayarishwa kwa ajili ya vitabu vya Sh. 2,094/- ambavyo waazimaji wake hawakujulikana waliko. Potevu hiyo ilifutwa.

(c) *Shule ya Sekondari ya Wasichana, Korogwe:—*

(i)—(iv): Hakuna maoni ya zaidi.

(d) *Butimba Chuo cha Elimu ya Taifa, Mwanza:—*

(i) na (ii) Hakuna maoni ya zaidi.

(iv) na (v) Hakuna maoni ya zaidi.

(vi) *Malinganisho kati ya Bakaa ya Vitabuni—Sh. 45,705/70:—*

Maelezo juu ya vifaa vya Sh. 37,289/85 yaliwasilishwa Uhakikimali.

(vii) *Mzabuni:—*

(a) *Deni la—(Sh. 13,555/75-):—*
Mzabuni alilipa deni la Sh. 3,683/25.

(viii) na (xi) Hakuna maoni ya zaidi.

(c) *Upotevu wa Vifaa—(Sh. 286,362/-):—*

(i) *Mazengo Shule ya Sekondari, Dodoma.*
Hakuna maoni ya zaidi.

(ii) *Folk Chuo cha Maendeleo, Tabora—(Sh. 176,223/-):—*

Wizara inawasiliana na Mwanasheria Mkuu juu ya hukumu aliyopewa Ndugu Charles Sambula, kwani amehukumiwa kifungo lakini hakupewa amri ya kuufidia upotevu huo.

(iii) *Mwenge Shule ya Sekondari—Singida—(Sh. 10,230/-):—*
Hakuna maoni ya zaidi.

(iv) *Kazima Shule ya Sekondari—Tabora—(Sh. 22,673/-):—*
Wizara imeomba kibali cha kufuta upotevu huu.

(v) *Mirambo Shule ya Sekondari:—*

(a) *Pikipiki—(Sh. 15,000/-):—*

(b) *Vifaa—(Sh. 32,000/-):—*

Polisi haikufanikiwa kuwapata watu waliohusika katika wizi wa pikipiki na vifaa hivyo, Majalada ya upelelezi wa wizi huo yamefungwa. Watumishi wanne waliotuhumiwa katika upotevu wa kifungu (b) wameacha kazi. Wizara imeomba kibali cha kufuta potevu hizi.

(vi) *Shinyanga Shule ya Sekondari—(Sh. 10,000/-):—*

(vii) *Usagara Shule ya Sekondari—Tanga—(Sh. 7,443/-):—*
Hakuna maoni ya zaidi.

## FUNGU 48.—WIZARA YA UJENZI

**112.** *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 135:—*

Kikosi cha kufuati ia maswali ya Ukaguzi pamoja na Maagizo ya Kamati kilikwishaundwa kama Wizara ilivyoagizwa. Sasa yamesalia maswali 338 ambayo bado yanashughulikiwa. Maendeleo ya ujibuji yaangaliwe kwenye taarifa ya 1981/82.

**113.** *Matokeo ya Hesabu—Aya ya 136:—*

(a) *Hesabu ya kawaida—*

Maombi ya uhalalisho wa matumizi ya zaidi yalikwishapokelewa na HAZINA. Agizo la Kamati lilizingatiwa. Mwelekeo utazamwe katika hesabu za miaka ijayo.

(b) *Hesabu ya Maendeleo:—*

Hatua za kusawazisha deni la benki zilikwishachukuliwa na HAZINA.

**114.** *Masurufu na Karadha—Aya ya 137:—*

(a) *Karadha Binafsi—(Sh. 1,077,359/40):—*

Wizara imethibitisha kwamba taratibu za utoaji na urejeshaji wa karadha binafsi sasa unafuatwa inavyostahili na kwamba mchanganuo wa karadha zisizorejeshwa ulikwishatayarishwa na kuwasilishwa UKAGUZI.

(b) *Karadha Aina Nyingine—(Sh. 5,314,378/30):—*

Wizara imethibitisha kuwa mchanganuo unaoonyesha Wizara na Mashirika yanayodaiwa ulikwisha tayarishwa. Ufuataliaji wa marejesho unaendelea.

(c) *Warrant of Funds:—*

Suala hili bado linashughulikiwa na HAZINA kupata ufumbuzi wa jumla kwani linazihusu Wizara nyingi.

(d) *Masurufu —(Sh. 25,480,637/70):*

(i) *War Effort—(Sh. 65,357/-):—*

Wizara bado inafanya juhudi za kushughulikia hesabu hiyo.

(ii) *Standing Imprests—(Sh. 65,557/-:—*

Marejesho ya masurufu hayo yanafuatiliwa na Wizara. Maendeleo ya marejesho yaangaliwe katika hesabu za miaka ijayo.

(iii) Masurufu ya Safari Sh. 9,758,193·15:—

Makusanyo ya masurufu yanaendelea. Wizara imethibitisha kuipatia UKAGUZI mchanganuo mpya wa masufuru yasiyorejeshwa.

**115.** *Hali ya Uwekaji Hesabu na Shahada ya Usahihi—Aya ya 138:—* Hatua za kurekebisha hali zinaendelea kuchukuliwa na Wizara. Matokeo yaangaliwe katika hesabu za miaka ijayo.

**116.** *Matumizi yasiyokuwa na Nyaraka na yenye Hati Pungufu—Aya ya 139:—*Wizara imetoa taarifa kwamba hati za matumizi yasiyokuwa na nyaraka zenye thamani ya Sh. 889,737·35 zimekwishapatikana na kwamba imebaki bakaa ya Sh. 3,749,018·20 ya matumizi hayo. Vile vile taarifa hiyo imeeleza kwamba maswali matano yahusuyo matumizi yenye hati pungufu yenye thamani ya Sh. 335,347·40. yamekwishajibiwa hivyo kubakiza maswali 16 yenye thamani ya Shs. 5,892,681·80. Juhudi za kutafuta nyaraka/hati zinazohusika zinaendelea. Maendeleo ya ujibuji yaangaliwe kwenye hesabu za mwaka 1981/82.

**117.** (a) *Malipo kwa Ankra Vifaa Sh. 18,464,453/—Aya ya 140:—* Malipo hayo bado yanafuatiliwa. Pia Wizara imeeleza kuwa imetoa waraka kwa maafisa wote kuacha mtindo wa ununuzi wa vifaa kwa kutumia ankra vifaani. Matokeo ya hatua hiyo yaangaliwe kwenye hesabu za miaka ijayo.

(b) *Nunuzi Bila Idhini Maalum—Sh. 1,177,102·25:—*Matokeo ya uchunguzi wa Polisi bado hayajapatikana.

**118.** *Gharama Zingeepukika na pia Malipo Zaidi katika Ukodishaji Gari Aya ya 141:—*Wizara imetoa taarifa kwamba fedha yote iliyolipwa zaidi ilikwisha katwa kwenye malipo ya mzabuni.

119. *Malipo Zaidi kwa Contractor—(Sh. 78,975/-)—Aya ya 142:—* Marejesho ya fedha hiyo bado yanafuatiliwa na Wizara.

120. *Gharama za Malazi Hotelini kwa Wataalam Baadhi Zingeweza kuepukika—Aya ya 143:*—Wizara ilizingatia onyo la Kamati na kuahidi kuwa waangalifu siku zijazo. Pia Wizara imeeleza kwamba karibu wataalam wote wanaohusika sasa wamepatiwa nyumba za Serikali.

121. *Ununuzi Usio wa Busara—(Sh. 5·12m/-)—Aya ya 144:*—Mtambo huo haujafanya kazi kwa sababu "generator" iliyopokelewa bado inajengwa. Vilevile suala la marejesho ya Sh. 700,000/- bado linafuatiliwa kwa Mwanasheria Mkuu.

122. *Ujenzi wa Barabara Inayokwenda Bandarini (Port Access Road) Aya ya 145:—*

(a) *Kipunguzo Bei (Discount) Kimepokelewa Pungufu—(Sh. 1·4 milioni):* Suala hili sasa limo mikononi mwa Mwanasheria Mkuu.

(b) *Madai kutokana na Safari ya Tanzania Kushuka Thamani yake (Sh. 4·12m/ au DMS 1·22 milioni):*—Wizara haijathibitisha kuipatia UKAGUZI nakala za mawasiliano kati yake na HAZINA kama ilivyoagizwa.

(c) *Malipo ya Madai kwa Gharama zilizofanyika Ziada—(Sh. 19·19 milioni):*—Uchunguzi zaidi bado unafanywa kuhusu suala hili.

123. *Ujenzi wa Kirumi Bridge—Aya ya 146:*—Wizara iliyazingatia maonyo ya Kamati. Ni matumaini ya HAZINA kwamba hali itageuka kuwa nzuri miaka ijayo. Vilevile Wizara imethibitisha kuwa imetengeneza mchanganuo wa malipo yote ya ziada na kuuwasilisha UKAGUZI.

124. *Fifth Highway Project—Aya ya 147:—*

(a) Kutumika kwa Wataalam (Personnel Utilisation):—Suala la nyongeza za mishahara ya wataalam wanaohusika limepelekwa Utumishi na Wizara. Uamuzi bado unangojewa.

125. *Malipo Mbele Yasiyo Sawa (Sh. 2·3 milioni) na malipo Ziada—(Sh. 493,920/-):—Kwa ununuzi wa Changarawe—Aya ya 148:*—Suala hili zima lilikwishakabidhiwa kwa Kikosi cha Kuzuia Rushwa tangu mwezi Machi 1983. Matokeo ya Uchunguzi wa Kikosi hicho bado yanasubiriwa

126. *Fourth Highway Project Passages to Experts and Their Families—(Sh. 2·82 milioni):—Aya ya 149:*—Wizara imeeleza kwamba mchanganuo wenye maelezo kamili ulikwishatolewa kwa UKAGUZI. Maoni ya UKAGUZI yanangojewa.

127. *Malimbikizo ya Maduhuli—(Sh. 8,678,848/90)—Aya ya 150:—* Makusanyo ya malimbikizo ya maduhuli yalifikia Sh. 1,607,930·20 hadi mwezi Juni 1983. Bidii za kufuatilia malimbikizo hayo zinaendelea.

128. *Mfuko wa Bohari ya Serikali—Aya ya 151:—*

(a) *Fedha Zinazodaiwa Wizara n.k.—(Sh. 352·87 milioni):*

(b) *Madai ya Mfuko Nchi za Ng'ambo—(Sh. 22·74 milioni):*

Wizara haijatoa taarifa zaidi juu ya masuala haya kuonyesha kama yamekuwapo mafanikio au hapana.

(c) *Usuluhisho wa Hesabu ya Benki:*
Hakuna maoni zaidi.

129. *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 152:—*

(a) *Potevu za Vifaa:*

Ujenzi Dar es Salaam.

(ii) *Self-Starter and Tarpauline for STF 483 (Isuzu)—(Sh. 20,000/-):*
Upelelezi wa Polisi bado unaendelea.

Ufundi Dar es Salaam.

(iv) *Peugeot GTC 426—(Sh. 12,000/-):*
Mapendekezo ya Wizara bado yanashughulikiwa na UHAKI-KIMALI.

(v) *Adding Machine—(Sh. 6,500/-):*
Mhusika anakatwa Sh. 250/- kila mwezi. Hadi Novemba, 1983 deni lililosalia ni Sh. 3,250/-.

Bohari Kuu Dar es Salaam.

(vi) *Vipuri vya Magari—(Sh 5,306/10):*
Matokeo ya rufaa bado hayajajulikana. Wizara bado inafuatilia suala hili.

(vii) *Vifaa—(Sh. 209,710/70):*
Mapendekezo ya Wizara kuhusu ufidiaji wa hasara hii bado yanashughulikiwa na UHAKIKIMALI.

(ix) *Kilimanjaro International Airport—(Sh. 5,140/-):*
Haikuwezekana kupata fidia yoyote na upotevu huu umekwishafutwa.

(b) *Ajali za Magari ya Serikali:*

(ii) Gharama halisi bado kujulikana kwani magari yanayohusika hayajatengenezwa kwa sababu ya kukosekana kwa vipuri.
(iii) Wizara haijathibitisha kiasi ambacho Serikali imekwishafidiwa hadi sasa.

## FUNGU 49—WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO MIJINI

130. *Maswali ya Ukaguzi na Hali ya Uwekaji Hesabu—Aya ya 153:—*

Kati ya Hoja za Ukaguzi 171 zilizosalia wakati wa Kikao cha Kamati sasa zimesalia hoja 68 tu. Wizara inaendeleza juhudi za kujibu hoja hizo zilizosalia. Maendeleo yaangaliwe kwenye hesabu za mwaka 1981/82.

131. *Karadha za Binafsi na Masurufu—Aya ya 155:—*

(a) *Karadha za Binafsi Zinazodaiwa—(Shs. 71,107-05):*
Wizara haikutoa taarifa ya maendeleo ya suala hili.

(b) *Masurufu Yanayodaiwa:*
Maoni ni kama kwenye (a) juu.

132. *Mishahara Imelipwa Zaidi—Aya ya 156:—*

(a) *Malipo Zaidi—(Sh. 8,356.60):—*

Maoni ni kama kwenye aya 131 (a) juu.

133. *Madai Yenye Mashaka—Aya ya 157:—*

(a) (i)—(iii): Wizara imechukua hatua ya kukata fedha inayohusika kutoka kwenye mishahara ya walipwaji watatu kuanzia mishahara ya mwezi Desemba 1983 kwa Sh. 700/- kila mtu kwa kila mwezi.

(b) Hazina pia inasubiri kuona mabadiliko kwenye hesabu za 1981/82.

134. *Potevu Magari—Aya ya 158:—*

(a) na (b): Taarifa za upotevu zilitumwa HAZINA. Polisi haijatoa matokeo ya upelelezi wa wizi huo.

135. *Uchunguzi wa Mhakikimali—Aya ya 159:*

(b) *Ardhi Institute Tabora:*

Wizara imetoa taarifa kwamba vipengele vyote vya aya hii vimeshughulikiwa kikamilifu na majibu yametumwa Uhakikimali kuhakikiwa.

## FUNGU 51—WIZARA YA MAMBO YA NDANI

136. *Taahira Kuletwa Hesabu—Aya ya 160:—*

Wizara inawasiliana na Hazina juu ya kuigawa Wizara hiyo katika mafungu matatu (Votes) kwa lengo la kuharakisha uwasilishaji wa hesabu za kila mwaka.

(i) Wizara imezingatia onyo la Kamati.

(ii) Michanganuo ya karadha na masurufu ilitayarishwa na kuwasilishwa Ukaguzi.

(iii) Hesabu za Mfuko wa Polisi na Magereza pamoja na Hesabu za Mali na Dhima za Mifuko hiyo zilitayarishwa na kuwasilishwa Ukaguzi.

(iv) Mchanganuo wa hesabu ya Karadha zisizotozwa riba ulitayarishwa na kuwasilishwa Ukaguzi.

Wizara inafanya jitihada kutafuta hundi zilizolipwa zinazohusu Hesabu ya Maendeleo ili ziwasilishwe Ukaguzi.

137. *Masuali ya Ukaguzi—Aya 161:—*

Kati ya Masuali 499 ya 1974/75 hadi 1980/81 yaliyosalia, maswali 381 yalijibiwa na kubakia masuali 118 ya 1976/77 hadi 1980/81. Wizara imeshaunda Kamati ya kujibu hoja. Maendeleo ya ujibuji yatazamwe katika hesabu za 1981/82.

138. *Matokeo ya Hesabu—Aya ya 162:—*

(a) *Hesabu ya Kawaida:—*

Wizara ilithibitisha kuwa itazingatia agizo la Kamati.

(b) *Hesabu ya Maendeleo:—*

Maoni ni kama ya (a) hapo juu.

**139.** (a) *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka na Yenye Hati Pungufu—Aya ya 163:—*

Kati ya hoja 25 zinazohusu matumizi yasiyokuwa na nyaraka, 5 zilijibiwa na 20 zilibakia. Hoja 22 zilijibiwa kutokana na hoja 44 zinazohusu matumizi yenye hati pungufu. Maendeleo ya ujibuji yatazamwe katika mwaka 1981/82.

(b) *Malipo kwa Ankra Vifani:—*

Wizara ilibakiza kujibu hoja 19. Hoja hizo zimechanganuliwa na kupelekwa Ukaguzi.

**140.** *Masurufu na Karadha—Aya ya 164:—*

Wizara ilitayarisha na kuwasilisha Ukaguzi michanganuo ya karadha na masurufu kama Kamati ilivyoagiza. Wizara pia inazingatia maagizo ya Kamati juu ya tozo ya 10% kwa Watumishi wanaochelewesha kurejesha masurufu.

**141.** *Mishahara imelipwa Mara Tatu—(Sh. 36,288)—Aya ya 165:—*
Wizara ilijibu hoja iliyohusika.

**142.** *Malipo Yenye Shaka—Aya ya 166:—*
Wizara ilijibu hoja iliyokuwepo.

**143.** *Ujenzi wa Ofisi ya Idara ya Uhamiaji Arusha—Aya ya 168:—*
Kontrakta aliyepewa kazi hii awali alinyang'anywa. Wizara imempata Kontrakta mwingine na kazi inaendelea.

**144.** *Ununuzi wa Mashine za Mahindi (Maize Mills)—Sh. 237,496/—Aya ya 169:—*

Wizara ilizingatia agizo la Kamati. Mawasiliano bado yanaendelea kati ya Wizara hii na Hazina kuhusu uundaji wa Kamati ya Ununuzi wa Vifaa.

**145.** *Fedha (Sh. 14,705.20) Haikupokelewa—Aya ya 170:—*
Wizara inaendelea kuwasiliana na Hazina juu ya ufutaji wa hasara hii.

**146.** *Orodha ya Malimbikizo ya Maduhuli—Aya ya 172:—*
Wizara inawasiliana na Hazina juu ya ulipaji wa fedha hiyo.

**147.** *Corporation Sole (Magereza)—Aya ya 173:—*
Hesabu za Mashirika yote ziliwasilishwa Ukaguzi. Hivi sasa ipo Corporation Sole moja tu kwa Idara ya Magereza.

**148.** *Potevu za Fedha Taslimu—Aya ya 174:—*

(i) *District Police Kigoma—(Sh. 267,175.65):*

Wizara iliwasilisha Taarifa ya Upotevu wa fedha hiyo.

(ii) *District Police Mbing.—(Sh. 8,067.25):*

Hukumu ya Mahakama bado haijatolewa.

**149.** *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 175:—*

(a) *Police Maintenance Unit Dodoma:—*

Wizara ilitoa maelezo kwa Wahakikimali na suala linalohusika lilifungwa.

(b) *District Police Dodoma—(Sh. 80,000/-):—*

Maoni ni kama (a) hapo juu.

(d) *Police Training School—Moshi—(Sh. ·,872,919.95):—*

Maoni ni kama ya (a) hapo juu.

(e) *Ajuli Zinazohusu Magari ya Serikali:—*

(i) Wizara inaendelea kutekeleza agizo la Kamati.

(ii) Wizara iliwasilisha Hazina Taarifa za ajali.

(iii) Wizara inaendelea na uchambuzi wake ili kujua ajali zilizo-shughulikiwa kikamilifu na zile zilizosalia.

## FUNGU 52.—WIZARA YA AFYA

150. *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 176:—*

Kati ya maswali 801 ya miaka 1975/76 hadi 1980/81 ambayo hayakuwa yamejibiwa wakati wa Kikao cha Kamati kilichopita yamejibiwa maswali 89 hadi sasa na bado yamesalia Maswali 712. Maendeleo ya ujibuji wa maswali yaangaliwe kwenye taarifa ya mwaka 1981/82.

151. *Matumizi zaidi (Sh. 2,002,997.45)—Aya ya 177:—*

Wizara ilitekeleza maagizo ya Kamati. Mwelekeo wa matumizi uangaliwe katika hesabu za mwaka ujao.

152. *Usuluhisho wa Hesabu ya Benki na Shahada ya Usahihi—Aya ya 178:—*

Wizara ilikwishakamilisha usuluhisho wa hesabu na kuuwasilisha UKAGUZI.

153. *Karadha za Binafsi na Masurufu—Aya ya 179:—*

(a) Hoja tatu zihusuzo karadha za Sh. 363,304.50 zilikwishajibiwa na kuwasilishwa UKAGUZI.

(b) Hoja tano zihusuzo masurufu ya Sh. 1,278,064.05 zilikwishajibiwa na kuwasilishwa UKAGUZI. Hoja moja iliyosalia bado inashu-ghulikiwa.

154. *Upotevu katika Dhibiti ya Ulipaji Mishahara—Aya ya 180:—*

(d) Kati ya Sh. 4,576.50 zilizokuwa zimesalia wakati wa Kikao cha Kamati kilichopita, Sh. 2,590.70 zilikwisharejeshwa. Kiasi kilicho baki bado kinafuatiliwa.

(e) *Wizara imetoa taarifa kuhusu hali ya sasa ya madeni hayo kama ifuatavyo:—*

(i) Maafisa wanne wanaohusika wataanza kukatwa madeni yao kwa Sh. 500/- kila mwezi kuanzia mshahara wa Novemba, 1983 Wanadaiwa jumla ya Sh. 31,005.10

(ii) Waajiri mbali mbali wa sasa wa maafisa 12 wameandikiwa barua za kuwaomba kuwakata madeni wahusika. Majibu bado hayajapatikana. Wanadaiwa jumla ya Sh. 69,296.85. Ila afisa mmoja amekwishalipa Sh. 4,455/- na mwingine kiasi adaiwacho hakikutajwa.

(iii) Afisa mmoja anayedaiwa Sh. 1,468.50 hajulikani aliko.

(iv) Vile vile yuko afisa mmoja ambaye haijathibitishwa kama anadaiwa au hapana.

155. *Malipo Yasiyo Kawaida na Yenye Shaka—Aya ya 181:—*

(a) Ununuzi wa Dawa toka UNICEF—Sh. 162,800/- Onyo la Kamati lilizingatiwa na Wizara.

(b) *Ununuzi wa Tetracycline—Sh. 823,715.20:*

Wizara iliahidi kuimarisha utaratibu wake wa kupokea na kugawa madawa. Hali iangaliwe katika hesabu za miaka ijayo.

(c) *Ununuzi wa Gari—5ton Betford Lorry—Sh. 200,000/-:—*

Taarifa ya upotevu wa lori hilo ilikwishatayarishwa kama ilivyoagizwa

156. *Asilimia 15 Inayolipwa Amana kwa malipo ya Ununuzi kutoka Ng'ambo Sh. 251,980/—Aya ya 182:—*

Wizara kwa kushirikiana na HAZINA ilifanikiwa ama kurejeshewa fedha inayohusika au kupata maelezo ya kuridhisha kutoka Benki ya Taifa ya Biashara na kuyajibu maswali ya ukaguzi yanayohusika.

157. *Malipo kwa Ankra Vifani—Sh. 4,823,963.25—Aya ya 183:—*

Maswali 33 yenye thamani ya Sh. 2,181,571/- bado yanafuatiliwa.

158. *Gharama za Maendeleo Zisizorejeshwa—Aya ya 184:—*

Hadi sasa haijawezekana kuthibitisha kama maombi ya Wizara ya Sh. 124,505.95 na ya Sh. 154,196.85 yalipokelewa na HAZINA na kupelekwa UNICEF kudai marejesho ya fedha hiyo kwa kufuata utaratibu uliopo.

159. *Mara Hospital—Sh. 3,209,072/—Aya ya 185:—*

Wizara haijatekeleza ushauri wa Kamati.

160. *Direct to Project Foreign Aid—Sh. 4,421,166/—Aya ya 186:—*

Wizara imethibitisha kwamba hoja inayohusika ilikwishajibiwa na kufungwa na UKAGUZI.

161. *Maduhuli Yatokanayo na Madawa Yanayotengenezwa—Sh. 4,058,448.15—Aya ya 187:—*

Wizara imeeleza kwamba inasubiri kukamilika kwa ukaguzi wa hesabu za Kiwanda cha Madawa, Keko za mwaka 1981/82 kuleta mapendekezo yake HAZINA kama Kamati ilivyoshauri.

162. *Potevu za Fedha na Vifaa—Aya ya 188:—*

(a) *Wizi wa Kuponi za Mafuta ya Petroli, Mishahara Isiyolipwa Watumishi. Vifaa vya Kwenye Maabara ya Serikali:—*

(i) *Mishahara Isiyolipwa Watumishi—Sh. 12,375/:—*
Uchunguzi wa Polisi kuhusu kesi hii bado haujapatikana.

(ii) *Maduhuli Yanayokusanywa:—*
Hali ni kama ya (i) juu.

(iii) *Kuponi za Mafuta ya Petroli za Thamani ya Sh 80,000/-:—*

Hali ni kama ya (i) na (ii) juu.

(iv) *Vifaa Havimo Hesabuni—Sh. 69,272.80:—*

Hali ni kama ya (i)—(iii) juu.

(b) *Potevu ya Fedha Taslim Kutokana na Railway Warrants Zilizoibiwa Wizarani—Sh. 144,904.35:—*

Uchunguzi wa wizi huu pia haujakamilishwa na Polisi. Ila Wizara imeimarisha udhibiti wa utoaji wa hati hizo na ulipaji wake. HAZINA inatumaini kuwa hali kama hiyo haitarudiwa tena miaka ijayo.

**163.** *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 198:—*

(a) *Mirembe Hospital—Dodoma:—*

(i)—(iii): Majibu ya Wizara yamekwishatumwa UHAKIKIMALI na yangali yanahakikiwa.

(c) *Potevu za Vifaa:—*

(i) Upotevu huu bado unafuatiliwa na Wizara.

(ii) Hali ya upotevu huu ni kama ya (i) juu.

(iii) Upotevu huu umekwishafutwa kwa mujibu wa Kanuni za Fedha.

(iv) Wizara inawasiliana na UHAKIKIMALI kuhusu jinsi ya kulifunga suala hili.

(v) Wizara imethibitisha kuwatoza wahusika asilimia kumi (10%) ya mishahara yao ya mwezi mmoja.

(vi) Madai ya Wizara bado yanachunguzwa na UHAKIKIMALI.

(vii) Bado Wizara inafuatilia upotevu huu.

(viii) Upotevu huu umekwishafutwa kwa mujibu wa Kanuni za fedha.

## FUNGU 53.—WIZARA YA HABARI NA UTAMADUNI

**164.** *Taahira Kuletwa Hesabu—Aya ya 190:—*

(i) Orodha ya Hesabu ya Malimbikizo ya Maduhuli ya Serikali: Hakuna maoni ya zaidi.

(ii) Michanganuo ya masurufu pamoja na orodha za hesabu ya fedha zinazodaiwa ilitayarishwa na kupelekwa Ukaguzi.

**165.** *Maswali ya Ukaguzi —Aya ya 191:—*

Kwa sasa yamesalia kujibiwa maswali 6 ya Voti 53 na 14 ya Voti 61 ya miaka ya 1977/78 hadi 1980/81 kati ya maswali 133 ya tangu 1975/76—1980/81 yaliyobakia kujibiwa. Wizara imejitahidi kujibu maswali ya Ukaguzi ingawa haikufanikiwa kujibu maswali yote kama Kamati ilivyoagiza. Maendeleo ya Ujibuji yatazamwe katika hesabu za 1981/82.

166. *Mambo yanayoathiri Hesabu za Jumla na Orodha za Hesabu—Aya ya 192:—*

(a) Hesabu za Matumizi ya Kawaida;

(i) Gharama Halisi Zilizofanyika—Sh. 54,253,106/70:—

(3) Wizara ilikwisha chukua hatua thabiti.

(c) Wizara ya Utamaduni na Vijana (Fungu 61);—

Hesabu za jumla na orodha zake ziliwasilishwa Ukaguzi.

167. *Karadha za Binafsi—Sh. 104,769/65—Aya ya 193:—*

Majibu ya hoja ya Sh. 15,728/- yalipelekwa Ukaguzi.

168. *Matumizi yasiyokuwa na Nyaraka na yenye Hati Pungufu—(Sh. 2,158,722/75)—Aya ya 194:—*

Wizara iliwasilisha Ukaguzi majibu ya hoja zilizohusu matumizi yasiyokuwa na nyaraka ya Sh. 1,331,771/75. Zile hoja zilizohusu matumizi yenye hati pungufu ya Sh. 29,191/70 na malipo ya ankra vifaani ya Sh. 90,000/- zilijibiwa na kufungwa.

169. *Malipo Yasiyo ya Kawaida na Yenye Mashaka—Aya ya 195:—*

(b) Majibu ya hoja ya Sh. 200/- yaliwasilishwa Ukaguzi.

(c) Kiasi cha Sh. 4,024/60 kimerejeshwa. Wizara inaendelea kushughulikia bakaa la Sh. 510/80 lililosalia.

170. *Utovu wa Dhibiti ya Malipo ya Miradi—(Sh. 980,000/-)—Aya ya 196:—*

Wizara iliwasilishwa Ukaguzi maelezo ya matumizi ya Sh. 980,000/-.

171. *Ulegevu katika Dhibiti ya Ununuzi na Uwekaji Hesabu wa Vifaa Aya ya 197:—*

(b) Vifaa havikuingizwa madaftarini—Sh. 227,078/50:—

Maelezo yalitolewa na kuwasilishwa Ukaguzi kuhusu uwekaji wa hesabu za vifaa.

172. *Potevu za Fedha Taslimu—(Sh. 2,809/-)—Aya ya 198:—*

Wizara ilitayarisha Taarifa ya Upotevu huo.

173. *Ukaguzi wa Mhakikimali—Government Publishing Agency—Aya ya 199:—*

(i) Wizara ilitayarisha maelezo yaliyotakiwa, kisha yakawasilishwa Uhakikimali.

(ii) Wizara ilifanya jitihada za kuwataka wapokeaji wa Vifaa watie sahihi zao katika hati za upokeaji wa vifaa hivyo. Maelezo yameshatayarishwa na kuwasilishwa Uhakikimali.

(iii) na (iv) Majibu ya hoja yalitayarishwa na kuwasilishwa Uhakikimali.

## FUNGU 54.—WIZARA YA MIPANGO NA UCHUMI

174. *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 200:—*

Kati ya maswali 12 ya mwaka 1980/81 yaliyokuwa yamesalia wakati wa Kikao cha Kamati kilichopita ni maswali 2 tu ambayo bado yanashughulikiwa na Wizara. Japokuwa Wizara haikuweza kuyajibu maswali yote kwa tarehe iliyotolewa na Kamati lakini juhudi zake za kuyashughulikia maswali ya ukaguzi zimeonekana. HAZINA inampongeza Afisa Mhasibu na maafisa wake wanaohusika kwa kazi nzuri waliyoifanya.

175. *Matokeo ya Hesabu—Aya ya 221:—*

(a) *Hesabu ya Matumizi ya Kawaida—(Sh. 2,794,959.35):*

(b) *Hesabu ya Matumizi ya Maendeleo—Deni Benki—(Sh. 1,391,904.40):*

Hakuna maoni zaidi.

176. *Gharama za Malazi Hotelini hazikupokelewa—(Sh. 20,112/90)—Aya ya 204:—*

(a) Hakuna maoni zaidi.

(b) Ajali kwa Magari Sh. 22,462/-:—

Wizara imethibitisha kuipatia UHAKIKIMALI taarifa zote zilizotakiwa ili kuiwezesha kufuatilia fidia ya Shs. 22,462/-.

## FUNGU 56.—WIZARA YA MAJI NA NISHATI

177. *HAZINA itatoa maoni yake baada ya Kamati kuzijadili hesabu hizo na kutoa maagizo yake:—*

## FUNGU 58.—RADIO TANZANIA

186. *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 227:—*

Sasa yamesalia maswali 8 yasiyojibiwa. Pamoja na Idara kutoweza kujibu maswali yote ya ukaguzi kwa muda iliopewa na Kamati juhudi zake za kuyashughulikia maswali hayo zimeonekana. HAZINA inampongeza Afisa Mhasibu na maafisa wake wanaohusika kwa kuipa kazi hiyo uzito unaostahili.

187. *Matokeo ya Hesabu—Aya ya 228:—*

(a) Hesabu ya Matumizi ya Kawaida—Sh. 2,600,162/95:—

Idara ililizingatia onyo la Kamati.

188. *Karadha na Masurufu Yanayodaiwa—Aya ya 231:—*

(c) Accommodation Codes Zingine—Sh. 126,758.70:—

Hakuna maoni zaidi.

189. *Miscellaneous Deposits Account—Aya ya 232:—*

Hakuna maoni zaidi.

190. *Gharama za Ujenzi wa Booster Station Kigoma—(Sh. 450,000/-)—Aya ya 234:—*

Idara imetoa taarifa kwamba maelezo ya Sh. 400,000/- yamekwisha patikana. Sh. 50,000/- zilizosalia bado zinazofuatiliwa.

191. *Kodi ya Nyumba—(Sh. 3,549/50)—Aya ya 235:—*

Idara inaendelea kufuatilia malipo ya deni hili.

## FUNGU 59—WIZARA YA USTAWISHAJI MAKAO MAKUU

192. *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 237:—*

Sasa yamesalia maswali 10 tu yasiyojibiwa ya mwaka 1978/79 hadi 1980/81. Ijapokuwa Wizara haikuweza kuyajibu maswali yote kwa ukamilifu kwa muda uliotolewa na Kamati, juhudi za kuyashughulikia maswali hayo zimeoonekana. HAZINA inampongeza Afisa Mhasibu na maafisa wake wanaohusika kwa kuipa kazi hiyo uzito unaostahili.

193. *Matokeo ya Hesabu—Aya ya 238:—*

(a) *Hessbu za Kawaida—*

Hakuna maoni zaidi.

(b) *Hesabu za Maendeleo (Sh. 18,142,492.45):—*

Deni la Benki lilithibitishwa kuwa halisi. HAZINA italiziba deni hilo kwa fedha ya Wizara ambayo haikuombwa kwa wakati wake. Wizara ilizingatia onyo la Kamati na kuahidi kuwa waangalifu zaidi miaka ijayo.

194. *Miradi Inayopata Misaada ya Nje—Aya ya 239:—*

Wizara ilitoa mchanganuo wa thamani ya vifaa vilivyopokelewa katika miaka 1979/80 na 1980 /81 na kuthibitisha kuwa thamani hiyo ililipwa HAZINA kwa mujibu wa Kanuni za Fedha.

195. *Masurufu na Karadha—Aya ya 240:—*

Karadha binafsi za Shs. 4,132/-, Karadha nyingine za Sh. 2,485/- na Masurufu ya Sh. 32,071/50 yamethibitishwa na Wizara kuwa yamekwisharejeshwa. Makato ya marejesho yanaendelea kufanywa kutoka kwenye mishahara ya wahusika.

196. *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka na Yenye Hati Pungufu—Aya ya 241:—*

Wizara imetoa taarifa kama ifuatavyo:—

Matumizi yasiyo na Nyaraka—Sh. 2,500/- zitaonyeshwa kwenye "Footnotes" za hesabu za 1983/84.

Matumizi yenye Hati Pungufu—Sh. 13,141/- hati zake zimepatikana. Kiasi kilichosalia bado kinashughulikiwa.

Malipo Batili—Sh. 8,411/50 zimekwisharejeshwa. Kiasi cha Sh. 14,183.50 bado kinafuatiliwa.

197. *Hesabu ya Mali na Dhima—Aya ya 243:—*

Hakuna maoni zaidi.

198. *Potevu ya Fedha—Aya ya 245:—*

Matokeo ya kesi ya upotevu wa Sh. 22,700/- bado hayajapatikana. maana kesi bado iko Mahakamani. Wizara inafuatilia kesi hiyo.

Wizara imethibitisha kulipa fidia ya Sh. 352,400/-. Juhudi za kuwatafuta wahusika wengine ili walipwe haki zao zinazendelea kufanywa.

## FUNGU 62—WIZARA YA MAWASILIANO YA UCHUKUZI

199. *Masuali ya Ukaguzi—Aya ya 246:—*

Wizara imetoa taarifa kwamba sasa yamesalia maswali manane (8) tu ambayo bado yanashughulikiwa. Juhudi za Wizara za kushughulikia maswali hayo zimeonekana na HAZINA inampongeza Afisa Mhasibu na maafisa wake wote wanaohusika.

200. *Mambo Yanayoathiri Hesabu za Jumla na Orodha Zake—Aya ya 247:—*

(a) Afisa Mhasibu alilizingatia onyo la Kamati na kuahidi kuwa mwaangalifu zaidi miaka ijayo.

(b) *Matumizi ya Maendeleo:—*

Wizara iliahidi kuzingatia taratibu za kihasibu zinazohusika miaka ijayo.

(c) *Warrant of Funds:—*

Wizara ilikiri kosa na kuahidi kutolirudia tena miaka ijayo.

(d) *Masurufu Yanayodaiwa:—*

Usuluhisho wa hesabu za masurufu sasa umekamilika hadi Juni 1982. Ukataji wa marejesho unaanza Januari, 1984.

(e) *Karadha za Binafsi:—*

Hali ni kama ya (d) juu.

**201.** (a) *Malipo ya Ovataimu Yasiyo Kawaida—Aya ya 248:—*

Wizara imethibitisha kwamba sasa inalipa ajira kwa kufuata Kanuni za Utumishi/Fedha.

(b) *Malipo ya Chakula kwa Watumishi wa DCA na MET:*

Wizara bado inawasiliana na Utumishi kuhusu suala hili.

(c) *Posho ya Ushushaji Ndege:—*

Hakuna maoni zaidi.

**202.** (a) *Ununuzi wa Karatasi na Vifaa Vingine Usio wa Kawaida:— Sh. 4,860,085/—Aya ya 249:—*

(i)—(iii) Wizara ilikwishashughulikia kikamilifu maswali mengi ya Ukaguzi yahusuyo mada hii. Yamesalia maswali manne tu ya 1980/81 ambayo bado yanafuatiliwa.

(b) *Ununuzi wa Mafuta Sh. 652,675/45:—*

Wizara imeahidi kutorudia mtindo wa kununua petroli kwenye vituo visivyokuwa na zabuni.

**203.** (a) *Utengenezaji wa Magari Kwenye Gereji za Watu Binafsi—Sh. 1,325,536/45—Aya ya 250:—*

Onyo la Kamati lilizingatiwa na Wizara.

(b) *Ukodishaji wa Magari—Sh. 276,741/-:—*

Wizara imeahidi kuzingatia taratibu za kukodi magari miaka ijayo.

(c) *Marejesho ya Gharama za Kukodi Teksi:*

Fedha iliyolipwa bila kuwa halali inakatwa kwenye mishahara ya wahusika.

**204.** *Ulegevu Katika Kupokea Maduhuli ya Serikali—(Sh. 11,263,831/15)—Aya ya 251:—*

Wizara bado inalifuatilia suala hili kwa kushirikiana na vyombo vingine vinavyohusika.

**205.** *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 252:—*

Majibu yalikwishawasilishwa UHAKIKIMALI.

## FUNGU 63.—KAMATI YA RAIS YA MASHIRIKA YA UMMA

**206.** *Matumizi Zaidi—Aya ya 253:—*

Afisa Mhasibu alilizingatia onyo la Kamati. Mwelekeo wa matumizi uangaliwe katika hesabu za miaka ijayo.

## FUNGU 64.—WIZARA YA MADINI

**207.** *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 254:—*

Juhudi za kujibu maswali hayo zinaendelea. Maendeleo ya ujibuji yaangaliwe kwenye hesabu za mwaka 1981/82.

**208.** *Matokeo ya Hesabu—Aya ya 255:—*

Hakuna maoni zaidi.

**209.** *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka—(Sh. 198,885/15) na Yenye Hati Pungufu —(Sh. 32,595,339/60)—Aya ya 256:—*

Maswali ya ukaguzi yanayohusika bado yanahushughulikiwa. Maendeleo ya ujibuji yaangaliwe katika hesabu za mwaka 1981/82.

**210.** *Geosurvey Mineral Exploration—Ruzuku—Aya ya 258:—*

Wizara haijatoa taarifa ya utekelezaji wa agizo hili.

**211.** *Shahada ya Usahihi—Aya ya 259:—*

Hakuna maoni zaidi.

**212.** *Ukaguzi wa Mhakikimali—Madini Stores Dodoma—Aya ya 26:—*

Wizara haijatoa taarifa ya utekelezaji wa gizo hili.

## FUNGU 65.—WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO

**213.** *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 261:—*

Wizara bado inayashughulikia maswali hayo. Maendeleo ya ujibuji yaangaliwe kwenye hesabu za mwaka 1981/82.

**214.** *Hesabu za Jumla—Aya ya 262:—*

Hakuna maoni zaidi.

**215.** *Uhamishaji wa Fedha Bila Idhini—(Sh. 1,765,446/-)—Aya ya 263:—*

Wizara imekiri kwamba ilijichukulia madaraka ya kuingiza fedha hiyo kwenye akaunti ya amana badala ya akaunti ya maduhuli jambo ambalo ni kinyume cha Kanuni za Fedha. Sasa HAZINA imeamua kwamba fedha hiyo ihamishiwe kwenye akaunti ya Mfuko Maalum ambao umeanzishwa kwa ajili ya ununuzi wa madawa na vifaa vya Mifugo, hivyo kulifunga suala hili.

**216.** *Direct-to-Project Aid—Gharama Haimo Hesabuni—Aya ya 265:—*

Matokeo ya hatua za Wizara yaangaliwe katika hesabu za miaka ijayo.

**217.** *Miscellaneous Deposits Account—Aya ya 267:—*

Hakuna maoni zaidi.

**218.** *Buhuri Livestock Training Centre, Tanga—Aya ya 268:—*

UHAKIKIMALI inalishughulikia suala hili ipasavyo:

## III.—KURUGENZI ZA MIKOA

### FUNGU 70.—MKOA WA ARUSHA

**219.** *Maswali ya Mkaguzi—Aya ya 269:—*

Kati ya maswali 190 yaliyosalia maswali 67 yamejibiwa na kufungwa bado 123 ambayo yanaendelea kushughulikiwa.

**220.** *Matokeo ya Hesabu—Aya ya 270:—*

(a) Agizo la Kamati limezingatiwa.

(b) (i) Utaratibu uliosahihi wa kuhasibu misaada itolewayo moja kwa moja kwenye miradi sasa unafuatwa na Mkoa.

(ii) Hoja hii imeshughulikiwa inavyopaswa na kufungwa.

(iii) Hakuna maelezo zaidi.

**221.** *Masurufu na Karadha—Aya ya 272:—*

(a) Mkoa haujatoa maelezo ya kuridhisha kuhusu kipengere hiki.

(b) Mkoa umeeleza kuwa hadi tarehe 30/6/80 masurufu yaliyokuwa hayajarejeshwa ni Sh. 97,959/50. Na kati ya kiasi hicho, Sh. 81,411/40 zimerejeshwa na kubakiza Sh. 16,548/10 ambazo juhudi ya kuzikusanya zinaendelea.

**222.** *Malimbikizo ya Maduhuli ya Appropriation-in-Aid—(Sh. 2,250,355/55)—Aya ya 273:—*

Mkoa umeeleza kuwa katika kuchunguza suala hilo umegundua kuwa umekuwa na malimbikizo makubwa kwa sababu kiasi walichokadiria kukusanya kimejumlisha maduhuli ambayo yanahusu Wizara nyingine kama vile Maliasili. Makosa hayo yatarekebishwa katika makadirio ya miaka inayofuata.

Kuhusu malimbikizo ya UPE juhudi zimefanywa za kuwaelemisha Wazazi pamoja na Walimu Wakuu wa Shule za Msingi juu ya umuhimu wa Wazazi kulipa michango hiyo.

**223.** *Manunuzi Yasiyokuwa na Nyaraka na Yenye Hati Pungufu—Aya ya 274:—*

(a) Hoja zote zilizosalia zimejibiwa na kufungwa.

(b) Hati za thamani ya Sh. 58,308/05 bado zinatafutwa.

**224.** *Malipo Yasiyo Kawaida na/au Yenye Mashaka, Matengenezo ya Gari—(Sh. 172,643/35)—Aya ya 275:—*

Mkoa umeridhishwa na hatua zilizochukuliwa kusuluhisha suala hili, na Hazina haina maoni zaidi.

**225.** *Kupokelewa kwa Kodi ya "With holding Taxi"—(Sh. 21,835/50)—Aya ya 276:—*

Agizo la Kamati limezingatiwa.

**226.** *Ulegevu Katika Dhibiti za Ununuzi wa Vifaa na Uwekaji wake—Aya ya 277:—*

(a) Vifaa vya thamani ya Sh. 124,405/- vimethibitika kupokelewa na kuingizwa daftarini.

(b) (i) Mkoa ulifanya uchunguzi na kuridhika kuwa taratibu za utunzaji vitabu vya madawa ulikuwa hauridhishi. Ha i hiyo sasa imerekebishwa, na sasa "ledgers" zinatunzwa mpaka kwenye Tarafa ambako ndiko usambazaji kwa wafugaji umefanywa.

(ii) DADO Hanang (Sh. 93,834/20).

Vifaa vya thamani ya Sh. 38,034/20 vimepatiwa maelezo ya kuridhisha.

(iii) D.W.E. Hanang (Sh. 7,582/30).

Vifaa vya thamani ya Sh. 38,000/- vimepatiwa maelezo ya kuridhisha.

(iv) District Engineer Hanang (Sh. 78,433/80).

Suala hilo bado linashughulikiwa.

**227.** *Kodi za Nyumba Hazikupokelewa—(Sh. 223,970/20)-Aya ya 278:—*
Malimbikizo yote yamekusanywa, na suala hili sasa limefungwa.

**228.** *Mauzo ya Mbegu za Kilimo—Sh.128,218/70—Aya ya 279:—*
Mkoa umeamua kuwakata Mabwana Shamba waliohusika na mauzo hayo Sh. 21,128/70 kufidia deni hilo, kiasi kilichosalia Sh. 25,277/50 ni thamani ya mbegu zilizouzwa kwa Halmashauri za Vijiji, na Mkoa unaendelea kufuatilia suala hilo ili kuhakikisha kuwa vijiji viavyohusika vinarejesha fedha hizo.

**229.** *Potevu za Fedha na Vifaa—Aya ya 280:—*

(a) (i) Matokeo ya kesi hiyo bado kupatikana;

(ii) Mtuhumiwa alifungwa miaka 5 na kuamriwa kurejesha fedha hizo atakapoachiliwa. Hajaachiliwa bado.

(iii) Mhusika bado yuko kifungoni;

(b) (i) Watuhumiwa katika kesi hiyo wote wametoroka na Polisi bado wanawatafuta. Agizo la Kamati kuhusu uwekaji bora wa madawa limezingatiwa.

(ii) Afisa Mhasibu aliuandikia upotevu huo taarifa ya upotevu na halafu kuifuta kulingana na kanuni za fedha. Kutokana na hatua hiyo suala hili sasa limefungwa na Hazina haina maoni zaidi.

(iii) Mkoa umeeleza kuwa katika kuchunguza zaidi juu ya suala hili imegundulika kuwa vifaa vilivyopotea sasa ni "Washing basins" 7 tu za thamani ya Sh. 2,394/- na wala sio vifaa vya thamani ya Sh. 28,728/- kama ilivyoelezwa hapa awali katika taarifa ya ukaguzi. Dosari hiyo sasa imerekebishwa na taarifa mpya ya upotevu imetumwa Ukaguzi na Hazina. Hatua za kusuluhisha suala hilo zinaendelea.

(iv) Mhusika na upotevu huo alitoroka na hadi sasa hajapatikana.

(v) Mhusika aliachiwa huru na Mahakama na hatimaye Mkoa ulimchukulia hatua za kinidhamu na kumfukuza kazi.

230. *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 281:—*

(a) (i)—(v) Maelezo kuhusu vipengere hivyo yaliwasilishwa Uhakikimali kama Kamati ilivyoagiza.

(b)—(g) Maagizo ya Kamati yamezingatiwa.

## FUNGU 71.—MKOA WA PWANI

231. *Taahira Kuletwa Hesabu—Aya ya 282:—*

Mkoa umeahidi kuwasilisha hesabu za miaka inayofuata katika muda uliowekwa kisheria. Mafanikio yatizamwe kuanzia na hesabu za mwaka 1982/83.

Kuhusu masurufu na karadha za binafsi, juhudi ya kurejesha malimbikizo yaliyopo zinaendelea. Kiasi halisi kilichokusanywa kitaonyeshwa katika taarifa ya mwaka unaofuata.

232. *Maswali ya Ukaguzi na Taarifa Maalum—Aya ya 283:—*

Kati ya maswali 381 yaliyosalia, maswali 23 yamejibiewa na kufungwa, bado 358 ambayo Mkoa unaendelea kuyashughulikia.

Na kati ya zile Taarifa Maalum 7 ambazo zilikuwa bado kujibiwa, moja imekwisha kujibiwa, na zilizosalia zinaendelea kushughulikiwa.

233. *Matokeo ya Hesabu—Aya ya 284:—*

Hazina haina Maoni zaidi juu ya suala hili.

234. *Mambo Yanayoathiri Hesabu za Jumla na Orodha zake—Aya ya 285:—*

(a) Kati ya hoja 5 zilizosalia, hoja 2 zimejibiwa na kufungwa. Mkoa haukuonyesha ni nyaraka za kiasi gani zimepatikana kati ya nyaraka za thamani ya Sh. 31,187/20 zilizohojiwa.

(b) na (c) Maagizo ya Kamati kuhusu vipengere hivyo bado Mkoa haujayashughulikia kikamilifu.

(d) na (e) Mkoa bado unaendelea kushughulikia masuala hayo. Hatua kamili zilizofikiwa zitajulikana katika taarifa ya mwaka unaofuata.

235. *Usuluhisho wa Hesabu ya Benki na Shahada ya Usahihi—Aya ya 286:—*

(a) Kumekuwa na mafanikio kidogo katika usuluhishaji wa hesabu za Mkoa. Hatua zilizofikiwa zilionyeshwa katika taarifa iliyowasilishwa Ukaguzi.

236. *Ulegevu wa Dhibiti katika Ulipaji wa Mishahara, Posho,—n.k.—Aya ya 287:—*

(a) Kati ya kiasi cha Sh. 22,661/75 kilichosalia, kiasi cha Sh. 12,069/75 kimekusanywa, bado Sh. 10,592/-.

(b) Mkoa umeweza kujibu hoja 3 tu na kuzifunga. Kiasi kilichopatiwa maelezo hakikuelezwa.

237. *Nunuzi Zenye Shaka Zisizo za Kawaida—Aya ya 288:—*

(a) Hoja za thamani ya Sh. 1,206,281/30 zimejibiwa na kufungwa. Hoja za thamani iliyosalia zinaendelea kushughulikiwa.

(b) Mkoa haujatoa maelezo ya kuridhisha kuhusu kifungu hiki.

(c) Jibu ni kama (b) hapo juu.

(d) na (e) Mkoa haukutoa maelezo ya kuridhisha.

238. *Fedha Isiyopokelewa—(Sh. 109,323/80)—Aya ya 289:—*

Kiasi cha Sh. 2,362/- kilichokuwa kimesalia kimekusanywa.

239. *Malipo Yasiyo ya Kawaida na ya Shaka—Aya ya 290:—*

(c) Mkoa unaendelea kuwasiliana na Ukaguzi juu ya suala hili ili kuweza kulitolea maelezo ya kuridhisha.

240. *Potevu za Vifaa—(Sh. 83,731/-)—Aya ya 291:—*

(a) Upelelezi wa Polisi bado haujakamilika kuhusu suala hili. Mkoa unaendelea kulifuatilia.

241. *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 292:—*

(a) Mauzo ya thamani ya Sh. 41,923/15 yamekusanywa, na madawa ya thamani ya Sh. 61/10 yanaendelea kutafutwa.

(b) Hoja nane (8) zilizosalia bado zinaendelea kushughulikiwa.

## FUNGU 72.—MKOA WA DODOMA

242. *Kutowasilishwa Majibu UKAGUZI kabla ya Mkutano.*

Hakuna maoni juu ya suala hilo.

243. *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 293:—*

Kati ya maswali 115 yaliyosalia, Mkoa umeweza kujibu maswali 13 tu kubakiza 102. Hakuna sababu zilizotolewa za kushindwa kujibu maswali hayo yaliyosalia.

244. *Matumizi Ziada—Aya ya 294:—*

(a) na (b) Onyo la Kamati limezingatiwa. Matokeo yatizamwe katika mwaka unaofuata.

245. *Masurufu na Karadha Zinazodaiwa—Aya ya 295:—*

Hadi sasa kiasi cha Sh. 1,000/- kuhusu karadha za binafsi hakijarejeshwa. Kati ya masurufu ya Sh. 102,800/40 yaliyokuwa hayajarejeshwa, kiasi cha Sh. 28,607/75 kimepatikana, bado kiasi cha Sh. 74,192/65. Na kati ya karadha zingine za Sh. 81,000/85 zilizosalia Mkoa umeweza kukusanya Sh. 70,050/85 na kubakiza Sh. 10,950/-.

(b) Hazina haina maoni juu ya kipengere hicho.

246. *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka na Yenye Hati Pungufu—(Sh. 7,170,332/50)—Aya ya 296:—*

Kati ya kiasi cha Sh. 1,639,853/20 kilichosalia, matumizi ya Sh. 1,563,835/80 yamepatiwa maelezo ya kuridhisha. Mkoa unaendelea kutafuta nyaraka za thamani ya Sh. 76,017/40.

**247.** *Malipo Yenye Mashaka/Yasiyo Kawaida—Aya ya 297:—*

(b) Hazina haina maoni zaidi juu ya suala hilo.

(c) Utaratibu huo unafuatwa.

(d) Baada ya kuwasiliana na Wazo Hill Mkoa umehakikishiwa kuwa, kiasi sahihi kilicholipwa wasafirishaji hao ni Sh. 11,564/-, na kiasi hicho kimerejeshwa na wasafirishaji hao na hoja kufungwa.

(e) Onyo la Kamati limezingatiwa.

**248.** *Ulegevu katika Dhibiti ya Ununuzi wa Vifaa na Uwekaji Hesabu wake—Aya 298:—*

(b) Kati ya Vifaa vya thamani ya Sh. 648,555/35 ambavyo havikuonekana katika madaftari, vifaa vya thamani ya Sh. 22?,606/40 vimethibitika kupokelewa. Mkoa unaendelea na juhudi ya kutafuta vifaa vilivyosalia.

(d) Ufuatiliaji wa taarifa hiyo ya potevu bado unaendelea:

**249.** *Ajali kwa Magari ya Serikali—(Sh. 238,541/50)—Aya ya 299:—*

Mkoa umeeleza kuwa umekwishatuma taarifa za ajali Hazina kama ulivyoagizwa na Kamati na kuwa watumishi waliohusika haukuwachukulia hatua za kinidhamu kwa sababu eti hawakupatikana na hatia mbele ya Mahakama. Mkoa ulikumbushwa kuwa hata kama watumishi hao waliachiliwa na Mahakama ulikuwa na uwezo wa kuwachukulia hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Civil Service Regulations za mwaka 1970.

**250.** *Madai—(Sh. 15,947,930/-)—Sio—(Sh. 15,949,755/35)—Aya ya 300:—*

(a) Kati ya Sh. 11,532,654/60 zilizosalia kiasi cha Sh. 6,368,236/60 kimekusanywa, bado Sh. 5,164,418/- ambazo Mkoa unaendelea na juhudi ya kuzidai.

(b) Mkoa umeweza kukusanya Sh. 1,196,245/50 na kubakiza kiasi cha Sh. 837,269/65 kati ya Sh. 2,033,515/15 zilizokuwa zimesalia kukusanywa.

**251.** *Hesabu za Amana zimelipwa Fedha kwa ziada—(Sh. 12,563,458/50)—Aya ya 301:—*

Usuluhisho wa hesabu hizo ulikamilishwa na kutumwa Ukaguzi, lakini hadi sasa Hazina haijapokea marejesho yeyote ya fedha za amana ambazo zimekaa katika Akaunti hiyo zaidi ya miaka 5 kama walivyoagizwa na Kamati.

**252.** *Mfuko kwa Matumizi Usio na Idhini—(Sh. 2,798,361/45)—Aya ya 302:—*

Kati ya Sh. 362,501/85 zilizokuwa zinadaiwa Sh. 154,722/25 zimekusanywa na kubakiza Sh. 207,779/60.

**253.** *Usuluhisho wa Hesabu ya Benki na Shahada ya Usahihi—Aya ya 303:—*

Hatua za kihasibu kuhusu hundi hizo zimekwisha chukuliwa na Mkoa.

**254.** *Potevu za Fedha Taslim—Aya ya 304:—*

(b) (i) Mhusika bado anatumikia kifungo cha miaka 8.
(ii) Kesi bado inaendelea Mahakamani.
(iii) Mhusika bado anatumikia kifungo.

255. *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 305:—*

(a) (i) Kazi hiyo haijakamilika kutokana kutokuwepo hati za awali za kununulia vifaa hivyo ambazo Mkoa unazihitaji kwa uthibitisho.

(ii) Vifaa vya thamani ya Sh. 26,911/05 vilivyokosekana vimetolewa taarifa ya upotevu;

(iii) Maelezo kuhusu vifaa hivyo yaliwasilishwa Uhakikimali.

(iv) Juhudi zinafanywa za kupata uthibitisho wa upokeaji wa vifaa vya thamani ya Sh. 95,305/70 ili kuviingiza vitabuni.

(v) Upelelezi wa Polisi kuhusu upotevu wa vifaa vya thamani ya Sh. 102,204/- unaendelea.

(vi) Mkoa umeshindwa kuyaingiza mafuta hayo katika "long sheet" na kwa kuwa kuna uthibitisho kuwa yaliingizwa katika leja umeaahidi kuwa hautarudia kosa hilo tena.

(vii) Vitabu hivyo bado kurejeshwa toka A.G. Chambers.

(viii) Jibu ni kama (vii) hapo juu.

(b) (ii) Vifaa vyote vilivyohojiwa havijatolewa maelezo.

(iii) Mifuko ya saruji ya thamani ya Sh. 12,096/- bado kurejeshwa.

(c) (i) Maelezo kuhusu matumizi ya vifaa vya thamani ya Sh. 59,759/- yalitolewa Uhakikimali.

(iii) Vifaa vyote vya thamani ya Sh. 174,014/- vilivyokuwa vimeazimwa vimerejeshwa.

(v) Vifaa vya thamani ya Sh. 667/- vimethibitika kupokelewa.

(vi) Agizo la Kamati limezingatiwa.

(viii) Vifaa vya thamani ya Sh. 10,111/50 bado kutolewa maelezo.

(d) Mkoa umeeleza kuwa kwa sababu ya kukosekana kumbukumbu umeshindwa kutoa mchanganuo huo.

## FUNGU 73.—MKOA WA IRINGA

256. *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 300:—*

Kati ya maswali 446 yaliyosalia ni maswali 13 tu yaliyojibiwa na kufungwa. Mkoa umeeleza kuwa mafanikio hayo madogo yanasababishwa na ukosefu wa kumbukumbu na kutopatikana malipo toka kwa wadaiwa mbalimbali.

257. *Mambo Yanayoathiri Hesabu za Jumla na Orodha zake—Aya ya 307:—*

(a) Mkoa umezingatia maagizo ya Kamati. Mafanikio yatizamwe katika miaka inayofuata.

(b) Mkoa umekusanya Sh. 7,253/- na kubakiza Sh. 36,160/40 kati ya kiasi kilichokuwa kimesalia kukusanywa.

(d) Kati ya kiasi cha Sh. 3,837,554/80 kilichokuwa kinadaiwa kiasi cha Sh. 1,900,665/60 kimerejeshwa, na salio la Sh. 1,936,889/20 linahusu madai ya vitu ambayo yamepelekwa Hazina kwa malipo.

(e) Kati ya kiasi cha 1,017,546/25 kilichosalia Mkoa umekusanya Sh. 713,074/20, bado Sh. 304,472/05.

(f) Mkoa umeeleza kuwa imeshindikana kukusanya ile bakaa ya Sh. 3,635,510/25 kutokana na ukosefu wa fedha. Mkoa uliagizwa kujibanabana kwenye mafungu yake ya mwaka unaofuata ili kufuta deni hilo. Vinginevyo fedha hizo zitakatwa na Hazina toka kwenye Exchequer Issues za mwaka huo, hatua ambayo inaweza kuathiri utekelezaji wa mipango yao kutokana na upungufu wa fedha. Kuhusu kiasi cha Sh. 589,385/- ambacho kilikuwa hakijarejeshwa, Mkoa haukutoa maelezo kuhusu kipengele hicho.

(g) (i) na (ii) Matumizi hayo yalihalalishwa na kuingizwa katika hesabu ya mwaka 1981/82.

258. *Utovu wa Dhibiti Katika Ulipaji Mishahara na Posho—Aya ya 309:—*

(a) Kiasi cha Sh. 2,700/- kati ya Sh. 5,880/- zilizokuwazimesalia, kimerejeshwa. Juhudi ya kukusanya fedha zilizosalia zinaendelea.

(c) Hoja hii sasa imefungwa baada ya Ukaguzi kupatiwa maelezo ya kuridhisha.

(e) Mchanganuo ulitayarishwa na kuwasilishwa Ukaguzi.

259. *Ulegevu kwenye Dhibiti ya Vifaa na Hesabu yake—Aya ya 310:—*

(a) Maelezo ya kuridhisha kuhusu malipo ya thamani ya Sh. 40,239/15 yametolewa Ukaguzi. Matumizi yaliyosalia yanaendelea kushughulikiwa.

(b) Vifaa vya thamani ya Sh. 300,826/10 vimethibitika kupokelewa na kuingizwa madaftarini na ukaguzi imepatiwa uthibitisho huo.

(c) Vifaa vya thamani ya Sh. 202,633/- vimethibitika kupokelewa na kuingizwa daftarini. Kuhusu tofauti ya vifaa vya thamani ya Sh. 284/- wahusika wanakatwa fedha hizo toka kwenye mishahara yao kufidia deni hilo.

260. *Malipo Yasiyo Kawaida na/au Yenye Shaka—Aya ya 311:—*

(d) Mkoa haukutoa maelezo kuhusu kipengele hicho.

261. *Hesabu ya Amana—Aya ya 312:—*

(a) Maoni ya Kamati yamezingatiwa.

(b) Suala hili bado linashughulikiwa.

262. *Ulegevu katika Dhibiti ya Ukusanyaji Maduhuli na kuyawasilisha Benki—Aya ya 313:—*

(c) (i) Maduhuli ya kiasi cha Sh. 60,193/30 hayajafanyiwa usuluhisho.
(iii) Kiasi cha Sh. 4,629/- pia bado kusuluhishwa.

(e) Kati ya kiasi cha Sh. 15,361/60 ambacho kilikuwa bado kukusanywa, kiasi cha Sh. 11,502/75 kimekusanywa na Mkoa na kubakiza Sh. 3,848/75.

263. *Mfuko wa Kuhudumia Magari—Aya ya 314:—*

(b) Mkoa umeeleza kuwa tofauti iliyopo kati ya jumla ya madeni ambayo Mfuko unadai na mchanganuo uliotolewa inatokan naa makosa katika hesabu. Pia Mkoa umeeleza kuwa kutokan naa ukosefu wa fedha hakuna madeni yoyote yaliyolipwa ama kku-u sanywa hadi sasa.

(d) Ukaguzi ulipatiwa uthibitisho wa upokeaji wa mafuta ya thamanii ya Sh. 18,900/-.

(e) Karatasi hizo zilipokelewa na kuingizwa daftarini.

264. *Potevu za Vifaa—Aya ya 316:—*

(b) (i) Hadi sasa Wizara inayohusika haijalipa madai hayo.

(ii) Hatua za kihasibu zimekwishachukuliwa kuhusu upotevu huo.

265. *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 317:—*

(c) (i)—(iv) Mkoa haukutoa maelezo kuhusu vipengele hivyo.

(d) Uhalalisho wa manunuzi hayo umeombwa toka Hazina.

(e) Mchanganuo kuhusu madawa hayo ulitolewa na kuwasilishwa Uhakikimali.

## FUNGU 74.—MKOA WA KIGOMA

266. *Hesabu za Jumla na Orodha zake—Aya ya 318:—*

V. *Hesabu za RIDEP.*

Hesabu hizo ziliwasilishwa Ukaguzi.

267. *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 319:—*

Kati ya maswali 213 yaliyosalia, maswali 56 yamejibiwa na kufungwa bado maswali 157 ambayo Mkoa unaendelea kuyashughulikia.

268. *Matokeo ya Hesabu—Aya ya 320:—*

(a) Matumizi hayo yameombewa uhalalisho wa Bunge.

(b) Hazina imekwisha toa mwongozo wa namna ya kushughulikia hesabu za vifaa vinavyotolewa moja kwa moja kwenye miradi na wafadhili. Ni matumaini ya Hazina kuwa makosa kama hayo hayatatokea tena ikiwa Mwongozo huo utazingatiwa ipasavyo. Kuhusu agizo la Kamati kuwa Mkoa uimarishe utunzaji wa vifaa vya miradi ili kupunguza uwezekano wa wizi, Mkoa haukutoa maelezo kuhusu kipengele hicho.

269. *Mambo Yanayoathiri Hesabu za Jumla na Orodha zake—Aya ya 321:—*

(c) Mkoa umethibitisha kuwa hesabu hizo zimeonyeshwa katika tanbihi ya hesabu za mwaka 1981/82.

270. *Usuluhisho wa Hesabu za Benki na Shahada ya Usahihi—Aya ya 322:—*

Usuluhisho wa hesabu hizo ulikamilishwa na kuwasilishwa Ukaguzi.

**271.** *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka na Yenye Hati Pungufu—(Sh. 7,580,288,80)—Aya ya 323:—*

Kati ya kiasi cha Sh. 3,976,380/60 kilichosalia, nyaraka za thamani ya Sh. 1,049,418/25 zimepatikana, nyaraka zilizosalia zinaendelea kutafutwa.

**272.** *Malipo Yasiyo ya Kawaida na/au yenye shaka—Aya ya 324:—*

(a) Hoja 9 zilizohusu matumizi ya Sh. 716,966/05 zimejibiwa na kufungwa.

(b) Hoja ya thamani ya Sh. 18,000/- imejibiwa na kuwasilishwa Ukaguzi.

**273.** *Ulegevu Katika Ununuzi na Utolewaji Hesabu ya Vifaa—Aya ya 322:—*

(a) Mkoa umethibitisha upokeaji wa vifaa vya thamani ya Sh. 56,500/-tu kati ya vifaa vya thamani ya Sh. 3,108,649/05 vilivyohojiwa. Juhudi za kufuatilia vifaa vilivyosalia zinaendelea.

(b) (i) Vifaa vya thamani ya Sh. 8,015/- vimethibitishwa kuingizwa daftarini.

(ii) Vifaa vya thamani ya Sh. 43,890/- pia vimethibitishwa kuingizwa daftarini.

(iii) Hadi wakati wa kuandika taarifa hii vifaa vya thamani ya Sh. 70,677/- havijapokelewa. Mkoa umewataka wadaiwa wawe wamelipia vifaa hivyo ifikapo Desemba 1983, au utawafungulia mashtaka.

(iv) Kati ya vifaa vya thamani ya Sh. 227,662/- vilivyohojiwa, vifaa vya thamani ya Sh. 201,542/- vimethibitika kupokelewa na kuingizwa daftarini, na vifaa vya thamani ya Sh. 26,120/- havijapokelewa.

(v) Vifaa vyote vimeingizwa daftarini.

(vi) Leja iliyokuwa Polisi imerejeshwa na vifaa hivyo sasa vimekwishahakikiwa na Wakaguzi.

(ix) Hadi sasa vifaa vya thamani ya Sh. 25,671/- havijapokelewa na Mkoa umechukua hatua za kumshitaki mhusika. Vifaa vya thamani ya Sh. 4,304/- viliibiwa, na wahusika wamefikishwa Polisi.

(xii) Hadi sasa vifaa hivyo havijapokelewa na wahusika wameshtakiwa Polisi.

(xiv) Vifaa vya thamani ya Sh. 44,619/50 vimepokelewa na kuingizwa daftarini.

(xvi) Vifaa hivyo vimeingizwa daftarini.

(xx) Hoja inayohusika imejibiwa na kufungwa.

(xxii) Vifaa vya thamani ya Sh. 32,238/- vimeingizwa daftarini.

(xxiii) Mbao za thamani ya Sh. 6,838/20 zimepokelewa.

(xxiv) Hatua za kukomesha wizi huo zimechukuliwa, pia Mkoa umeandika taarifa ya potevu kuhusu kopo 100 za madawa zilizopotea.

(c) (i) Kiasi cha Sh. 30,100/- kimekwisharejeshwa, na juhudi za kupata kiasi kilichosalia zinaendelea.

(iv) Mhusika amefunguliwa mashtaka na matokeo ya kesi hiyo bado kupatikana.

(v) Hazina haina maoni zaidi juu ya suala hili.

(vi) Hazina haina maoni zaidi juu ya suala hili.

(vii) Mkoa umeandika taarifa ya potevu baada ya kukosa nyaraka za kuthibitisha upokeaji wa vifaa vya thamani hiyo.

(viii) Hadi sasa vifaa vya thamani ya Sh. 35,375/- havijapokelewa.

(ix) L.P.O. Na. 904409 ya tarehe 26/9/81 ilinunulia batteries za thamani ya Sh. 605/05 ambazo hadi sasa hazijapokelewa, kutoka R.T.C. Kasulu. Shirika hilo limetakiwa kurejesha fedha hizo. L.P.O. 904298 ya 29/6/81 ilifutwa na Wakaguzi wameelezwa kuwa hakuna malipo yaliyofanyika.

(x), (xi), (xii) na (xiii)—Ukaguzi ilitoshelezwa juu ya masuala hayo.

(II) Vifaa vya thamani ya Sh. 4,000/- vimepokelewa, na madai ya vifaa vya thamani ya Sh. 19,600/- yamefikishwa Mahakamani

(d) Shirika la Biashara la Mkoa wa Kigoma limetakiwa kurejesha fedha ikiwa litashindwa kutoa Saruji ya thamani hiyo. Hadi sasa hakuna fedha wala Saruji iliyopokelewa.

(f) (ii) Manunuzi hayo bado kupatiwa usuluhisho wa Hazina.

274. *Ukodiji wa Magari—(Sh. 330,992/-)—Aya ya 326:—*

(a) Hoja ya thamani ya Sh. 74,600/- iliyokuwa imesalia imejibiwa na kufungwa.

(b) Utaratibu wa kutengeneza magari nje ya karakana za Serikali, unazingatiwa, na hoja zilizokuwa zinahusika na kipengele hiki zimejibiwa na kufungwa.

275. *Ulegevu katika Dhibiti ya Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali—Aya ya 327:—*

(b) Kiasi cha Sh. 791,541/85 kimekusanywa kati ya Sh. 1,899,892/70 zilizokuwa hazijakusanywa. Juhudi zinaendelea za kukusanya kiasi kilichosalia.

276. *Potevu za Fedha na Vifaa—Aya ya 328:—*

(a) (i) Kesi hiyo imeanza upya baada ya watuhumiwa kuachiwa huru na Mahakama. Taarifa ya upotevu imewasilishwa Hazina.

(ii) Aliyehusika na wizi wa Sh. 2,280/- hajapatikana, na juhudi za kumtafuta zinaendelea.

(iii) Mhusika na wizi huo alipatikana na hatia na kufungwa jela miaka 5.

(b) (ii) Wahusika waliachishwa kazi baada ya kuachiwa na mahakama ya rufaa.

(iii) Mhusika amerejeshwa kazini, na anafidia upotevu huo kwa kukatwa Sh. 200/- toka kwenye mshahara wake kila mwezi.

(iv) Wahusika na wizi huo walifukuzwa kazi.

(v) Kesi hii ilifungwa na Polisi kwa kukosa ushahidi.

(vii) Kesi hii ilifutwa, na Hazina imeombwa kufuta upotevu huo.

277. *Ukaguzi wa Uhakikimali—Aya ya 329:—*

(a) (i) na (ii) Hazina haina maoni zaidi juu ya suala hili.

(iii) Vifaa vyote vya thamani ya Sh. 3,596,067/20 vimethibitishwa kupokelewa na kuingizwa daftarini.

(iv) Madaftari ya thamani ya Sh. 689,500/- yamethibitishwa kupokelewa na kuingizwa daftarini.

(b) (i) Vifaa vya thamani ya Sh. 19,964/50 vimepatiwa maelezo ya kuridhisha kuhusu matumizi yake.

(2) Madawa ya thamani ya Sh. 378,530/- yamepatiwa maelezo ya kuridhisha kuhusu matumizi yake.

(3) Vifaa vya thamani ya Sh. 6,646/- vimetolewa maelezo, vifaa vya thamani ya Sh. 8,453/50 havijapatikana.

(4) (i) Vifaa vya thamani ya Sh. 50,795/- ambavyo vilikuwa havijapokelewa sasa vimekwishapokelewa na kuingizwa vitabuni.

(ii) Maelezo kuhusu madawa yenye thamani ya Sh. 219,635/- yalitolewa kwa Wahakikimali.

## FUNGU 75.—MKOA WA KILIMANJARO

278. *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 330:—*

Maswali 166 kati ya 311 yamejibiwa na kufungwa.

279. *Matokeo ya Hesabu—Aya ya 331:—*

(a) na (b) Onyo la Kamati limezingatiwa.

280. *Usuluhisho wa Hesabu ya Benki na Shahada ya Usahihi—Aya ya 332:—*

(a) Usuluhisho wa hesabu ulitengenezwa na kuwasilishwa Ukaguzi.

(b) Orodha za Hesabu ya Mali na Dhima.
Orodha ilitayarishwa na kutumwa ukaguzi.

281. *Karadha na Masurufu—Aya ya 333:—*

(a) Kati ya Sh. 166,456/35 za karadha zilizokuwa zinadaiwa Sh. 79,862/25 zimekusanywa na kubakiza Sh. 86,593/70 ambazo zinaendelea kukatwa toka kwenye mishahara ya wahusika.

(b) Kati ya Sh. 669,157/25 za Masurufu zilizokuwa zinadaiwa Sh. 216,417/90 zimekusanywa na kubakiza Sh. 452,739/35 ambazo inaendelea kukusanywa.

282. *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka na Yenye Hati Pungufu ya (Sh. 7,779,489/-)—Aya ya 334:—*

(a) Kati ya nyaraka za thamani ya Sh. 1,878,701/65 zilizokuwa zinakosekana, nyaraka za thamani ya Sh. 1,587,449/20 zimepatikana.

(b) Nyaraka za thamani ya Sh. 2,408,329/55 zimepatikana kati ya nyaraka za thamani ya Sh. 2,907,548/90 zilizokuwa zinakosekana.

283. *Ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya ya Mwanga—Aya ya 335:—*
Uchambuzi wa matumizi ya ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya ya Mwanga umesababisha kurejeshwa kwa Sh. 63,729/00 ambazo zilikuwa zimelipwa zaidi kwa Mzabuni. Mkoa unaendelea kuwasiliana na Hazina ili kupata uhalalisho wa mikataba ya ujenzi ambayo ilitolewa kinyume cha utaratibu.

284. *Malipo Yasiyo Kawaida na/au Yenye Mashaka—Aya ya 336:—*

(a) Bidhaa za thamani ya Sh. 1,923,132/50 zimethibitishwa kupokelewa kati ya bidhaa za thamani ya Sh. 2,521,552/90 ambazo zilikuwa hazijapatiwa maelezo ya kuridhisha kuhusu upokeaji na matumizi yake.

(b) Mkoa ungali unawasiliana na Hazina kuhusu suala hilo.

(c) Suala hilo sasa limefungwa baada ya Mkoa kutoa maelezo ya kuridhisha Ukaguzi.

285. *Ajali kwa Magari ya Serikali—(Sh. 297,329/20)—Aya ya 337:—*
Agizo la Kamati limetekelezwa.

286. *Malipo ya Batili—(Sh. 92,901/50)—Aya ya 338:—*
Hoja hii imefungwa baada ya Mkoa kuipatia ukaguzi maelezo ya kuridhisha.

287. *Potevu za Fedha na Vifaa—Aya ya 339:—*

(a) Upotevu huo bado upo chini ya upelelezi wa Polisi.

(b) (i) Kesi hiyo imefungwa kutokana kukosekana ushahidi wa kutosha

288. *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 340:—*

(a) (i) Mkoa umethibitisha upokeaji wa vifaa vya thamani ya Sh. 175,446/20 vilivyokuwa vimesalia.

(v) Maelezo ya kuridhisha kuhusu vifaa hivyo yametolewa uhakikimali.

(c) Hakuna maoni zaidi.

(d) Madawa ya thamani ya Sh. 873,866/- yamethibitishwa kupokelewa, bado madawa ya thamani ya Sh. 11,320/- ambayo Mhakikimali Mkuu wa Serikali anaendelea kuyafanyia uchunguzi.

(e) Taarifa za Potevu zilitolewa na kuwasilishwa Hazina.

## FUNGU 76.—MKOA WA LINDI

289. *Kuchelewa kuwasilisha Majibu ya Taarifa ya Ukaguzi:—*
Onyo la Kamati limezingatiwa.

290. (a) *Taahira ya Kuletwa Hesabu—Aya ya 341:—*

(i) Mkoa umeeleza kuwa kazi ya kuchambua hesabu hizo ili kuzitarisha upya inaendelea.

(ii) na (iii) Hazina haina maoni kuhusu vipengele hivyo.

(iv) Hadi wakati wa kuandika taarifa hii usuluhisho wa hesabu hizo haujakamilishwa.

(b) *Usuluhisho wa Hesabu na Shahada ya Usahihi:*

Mkoa umeeleza kuwa usuluhisho wa hesabu ya matumizi ya kawaida kwa mwaka 1980/81 umefanywa hadi kufikia mwezi Machi 1981. Mkoa umeshindwa kufanya usuluhisho wa hesabu hizo hadi kufikia tarehe 30/6/81 kwa sababu ya Wilaya kushindwa kuwasilisha usuluhisho wa hesabu zao.

**291.** (a) *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 342:—*

Maswali 137 yamejibiwa na kufungwa kati ya maswali 525 yaliyokuwa yamesalia.

(b) Baadhi ya taarifa maalum za Ukaguzi zilizokuwa zimesalia zimejibiwa.

**292.** *Matokeo ya Hesabu—Aya ya 343:—*

(a) Hazina imezidi kuusisitizia Mkoa juu ya umuhimu wa kuzingatia viwango vilivyoidhinishwa na Bunge katika Bajeti. Mafanikio yatizamwe katika miaka inayofuata.

(b) Hoja kuhusu suala hilo bado kutolewa majibu.

**293.** *Karadha na Masurufu—Aya ya 344:—*

(a) Mkoa bado kukamilisha hesabu hiyo.

(b) Wenye malimbikizo ya masurufu wanaendelea kukatwa fedha hizo toka kwenye mishahara yao, na makato yanayofanyika ni pamoja na asilimia ya bakaa ya kila mwezi kulingana na kanuni za fedha.

(c) Jitihada ya kuwakata wahusika fedha hizo toka kwenye mishahara yao zinaendelea.

**294.** *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka na Yenye Hati Pungufu—(Sh. 11,543,065/20)—Aya ya 345:—*

Kati ya hoja 60 za thamani ya Sh. 1,779,214/15 zilizokuwa zimesalia kuhusu matumizi yasiyokuwa na nyaraka hoja 18 za thamani ya Sh. 675,565/20 zimejibiwa na kufungwa. Hoja 6 za thamani ya Sh. 58,361/- bado kupatiwa maelezo.

**295.** *Utovu wa Dhibiti Katika Ulipaji wa Mishahara, Posho na Kodi za Nyumba—Aya ya 346:—*

Kiasi sahihi kilichokuwa hakijarejeshwa ni Sh. 16,100/20 na siyo Sh. 96,100/20 kama ilivyoonyeshwa katika Taarifa ya Kamati. Kati ya kiasi hicho (Sh. 16,100/20), Sh. 902/95 zimerejeshwa, bado Sh. 15,197/25.

(b) Kiasi cha Sh. 2,832/25 kimerejeshwa kati ya Sh. 8,038/40 zilizokuwa imesalia. Hadi sasa Mkoa haujakusanya posho ya Sh. 2,505/- ambayo ililipwa marudufu kwa mtumishi mmoja.

(c) Fedha hizo bado kurejeshwa, na juhudi ya kuzipata zinaendelea.

(d) Kiasi cha Sh. 35,820/- kimekusanywa kati ya Sh. 39,570/- zilizokuwa hazijakusanywa.

(e) Kiasi cha Sh. 1,200/- zimekusanywa kati ya Sh. 5,242/50 zilizokuwa zimesalia.

296. *Malipo Yasiyo Kawaida na/au Yenye Shaka—Aya ya 347:—*

(a) Hoja za thamani ya Sh. 66,684/60 zimejibiwa na kufungwa, na zilizosalia zinaendelea kushughulikiwa.

(b) Hoja za thamani ya Sh. 88,345/- zimejibiwa na kufungwa; hoja moja ya thamani ya Sh. 42,001/- imepelekwa Ujenzi ili waishughulikie wao kwa sababu inahusu barabara ya Kibiti/Lindi, na hoja zilizosalia zinaendelea kushughulikiwa.

(c) Hoja zote 3 za thamani ya Sh. 10,267/60 zimejibiwa na kufungwa.

297. *Hesabu za Amana Zimelipwa Fedha kwa Zaidi—Aya ya 348:—*

Michanganuo ya hesabu hizo ilitengenezwa na kuwasilishwa Ukaguzi, na makosa yaliyobainika yamesahihishwa.

(b) Hazina haina maoni kuhusu kipengele hicho isipokuwa kueleza tu kuwa tumeuonya Mkoa kuacha mtindo huo.

298. *Ulegevu Katika Dhibiti ya Vifaa—Aya ya 348:—*

(a) Mkoa haujapokea vifaa hivyo wala thamani yake toka R.T.C. Lindi.

(b) (i) Madawati ya thamani ya Sh. 30,150/- yamepokelewa.
(ii) Vifaa vya thamani ya Sh. 80,790/- bado kupokelewa hadi sasa. Mkoa haukutoa maelezo kuhusu upokeaji na matumizi ya Saruji mifuko 1,414 yenye thamani ya Sh. 134,012/-.

299. *Ulegevu Katika Kudai fedha ya Serikali—(Sh. 2,947,179/65)—Aya ya 3 0:—*

Bills za thamani ya Sh. 903,934/65 zimekusanywa kati ya bills za thamani ya Sh. 1,576,260/90 zilizokuwa zimesalia kukusanywa. Ukusanyaji wa bills zilizosalia unaendelea.

300. *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 351:—*

(a) (i) Maelezo kuhusu vipuri hivyo yalipelekwa Uhakikimali.
(iv) Maelezo ya kuridhisha yaliwasilishwa Uhakikimali.
(vi) Mkoa haukutoa maelezo kuhusu kipengele hiki.

(b) (i) Mhusika hajalipa deni hilo.
(iii) Madawa ya thamani ya Sh. 135,550/- yametolewa maelezo kuhusu utumiaji wake.
(iv) Maelezo kuhusu matumizi ya madawa ya thamani ya Sh. 38,808/- yametolewa Uhakikimali.
(v) Hati za thamani ya Sh. 206,400/- bado kutiwa saini na wahusika kuthibitisha upokeaji wa madawa ya thamani hiyo.

(c) (ii) Vifaa vya thamani ya Sh. 10,991/20 bado kuthibitishwa kupokelewa.

(d) (i) Agizo la Kamati limetekelezwa.
(ii) Uchunguzi kuhusu suala hilo bado unaendelea.

## FUNGU 77.—MKOA WA MARA

301. *Kutowasilisha Majibu ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati Mkutanoni:—*

(a)—(c) Maagizo yote ya Kamati yametekelezwa.

302. *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 352:*

Kati ya maswali 799 yaliyokuwa yamesalia, maswali 524 yamejibiwa, bado 275 ambayo yanaendelea kushughulikiwa.

303. *Matokeo ya Hesabu—Aya ya 353:—*

(a) na (b) Mkoa haukutoa maelezo yoyote kuhusu aya hii, lakini inategemewa kuwa onyo la Kamati litazingatiwa. Mafanikio yatizamwe katika mwaka unaofuata.

304. *Usuluhisho wa Hesabu ya Benki na Shahada ya Usahihi—Aya ya 35-:—*

Mkoa umeithibitishia Hazina kuwa usuluhisho wa hesabu hizo ulifanyika kama Kamati ilivyoagiza, na wajibu wa kusawazisha hesabu za benki kila mwezi umetiliwa mkazo.

305. *Karadha na Masurufu—Aya ya 355:—*

Kiasi cha Sh. 233,373/90 kilichokuwa kimesalia sasa kimerejeshwa na mchanganuo wa masurufu, umetayarishwa na kuwasilishwa ukaguzi.

306. *Mambo yanayoathiri Hesabu za Jumla na Orodha Zake Aya ya 356:—*

(a) Mchanganuo wa malimbikizo ya maduhuli bado kutengenezwa na Mkoa haujatoa hesabu ya malimbikizo yaliyokusanywa.

(b) Hakuna maoni.

307. *Matumizi Yasiyokuwa na nyaraka (Sh. 3,204,975/25) na yenye Hati Pungufu—(Sh. 12,000,787/95):—*

Matumizi yasiyo na nyaraka ya thamani ya Sh. 893,870/05 bado kupatiwa maelezo, kuhusu matumizi yenye hati pungufu ya thamani ya Sh. 6,933,648/55, nyaraka za thamani ya Sh. 1,899,054/75 zimepatikana.

308. *Malipo yasiyo ya Kawaida na yenye Shaka—Aya ya 358:—*

(a) Matumizi ya thamani ya Sh. 52,956/30 yamepatiwa maelezo kati ya matumizi ya Sh. 182,239/30 yaliyohojiwa.

(b) Kiasi cha Sh. 148,157/50 kimetolewa maelezo kati ya kiasi cha Sh. 520,110/- kilichojiwa.

(c) Hoja za thamani ya Sh. 535,630/- zimejibiwa.

(d) Maelezo ya kuridhisha yametolewa Ukaguzi kuhusu kipengele hicho.

309. *Utovu wa Dhibiti ya vifaa—Aya ya 359:—*

(a) Vifaa vya thamani ya Sh. 278,350/45 vimethibitika kupokelewa na kuingizwa madaftarini, vifaa vya thamani ya Sh. 174,093/40 vimepotea na wahusika wametakiwa kuvitolea taarifa za potevu, na vifaa vya thamani ya Sh. 402/- havijapokewa toka RTC.

(b) Mkoa haujatoa uthibitisho kuhusu upokeaji na matumizi ya vifaa hivyo.

310. *Potevu ya fedha—(Sh. 347,150/50)—Aya ya 360:—*

(a) Kesi bado iko Mahakamani.

(b) na (c) Kati ya watumishi wawili waliohusika, mmoja amefukuzwa kazi na mwingine amevuliwa madaraka ya kuhusika na kazi za kihasibu.

(d) Kesi bado inaendelea Mahakamani.

**311.** *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 361:—*

Mchanganuo wa mauzo ya madawa ya thamani ya Sh. 921,444/- ulitolewa na kuwasilishwa Ukaguzi. Kati ya kiasi hicho imedhihirika kuwa mauzo ya madawa ya thamani ya Sh. 490,517/50 yamepokelewa na kulipwa Central Medical Stores, na kiasi cha Sh. 430,927/- bado kinadaiwa.

## FUNGU 78.—MKOA WA MBEYA

**312.** *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 362:—*

Kati ya masuali 296 yaliyosalia, maswali 46 yamejibiwa na kufungwa. Juhudi za kusuluhisha maswali yaliyobakia ambazo ni pamoja na kuwakata mishahara wote wanaodaiwa karadha na masurufu zinaendelea.

**313.** *Matokeo ya Hesabu—Aya ya 363:—*

(a) Maagizo ya Kamati kuhusu suala la kuepuka matumizi zaidi limezingatiwa na Mkoa. Matokeo yatizamwe katika hesabu zao za miaka inayofuata. Kuhusu suala la karadha na masurufu yasiyolipwa juhudi ya kurejesha fedha hizi na kufuta deni lililopo benki zinaendelea kama ilivyokwisha kuelezwa kwenye kifungu 312 hapo juu.

(b) Suala hili bado linashughulikiwa.

**314.** *Mambo Yanayoathiri Usahihi wa Hesabu za Jumla na Orodha za Hesabu—Aya ya 364:—*

(b) Hesabu hizo zilitengenezwa na kuingizwa katika tanbihi ya hesabu za mwaka wa fedha 1982/83.

(c) (ii) Baadhi ya potevu hizo zimeingizwa katika hesabu za mwaka 1982/83 na nyingine katika mwaka 1983/84.

(iii) Hatua zimechukuliwa kuziingiza potevu hizo katika hesabu za Mkoa.

(d) (i) Michanganuo ya Masurufu kwa miaka 1979/70 hadi 1980/81 na ya karadha hadi mwaka 1982/83 ilikwishatayarishwa na kuwasilishwa Ukaguzi. Imeshindikana na kutengeneza michanganuo ya madeni hayo kwa miaka 1976/77 mpaka 1978/79 kutokana na ukosefu wa kumbukumbu.

(ii) Mchanganuo wa madeni hayo bado kukamilika.

(e) (i) Mchanganuo kuhusu orodha hizo bado kutengenezwa.

(ii) Mkoa baada ya kupata maelezo ya kuridhisha toka Ukaguzi kuhusu bakaa hizo umekubali sasa kuziingiza katika hesabu yake ya Mali na Dhima, kwa mwaka unaofuata.

(iii) Mkoa unachukua hatua ya kuzifunga hesabu hizo na kurejesha fedha zisizotumika Hazina.

**315.** *Usuluhisho wa Hesabu ya Benki na Shahada ya Usahihi—Aya ya 365:—*

Hesabu za Mfuko wa Amana na "Plant and Transport Maintenance Fund" hadi 1981/82 na hesabu ya Mali na Dhima kwa mwaka 1981/82 zilitayarishwa na kuwasilishwa Ukaguzi. Usuluhisho wa hesabu za benki kwa mwaka 1980/81, ulikwishafanywa na kuwasilishwa Ukaguzi.

**316.** *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka na yenye Hati Pungufu—Aya ya 306:—*

(a) Nyaraka za thamani ya Sh. 36,079/75 zimepatikana kati nyaraka za thamani ya Sh. 117,565/75 zilizokuwa zinakosekana.

(b) Matumizi ya thamani ya Sh. 221,327/40 yamepatiwa maelezo ya kuridhisha.

(c) Vifaa vya thamani ya Sh. 269,842/45 vimethibitika kupokelewa.

**317.** *Malipo Batili—(Sh. 287,102/50)—Aya ya 367:—*

Malipo Batili ya Kiasi cha Sh. 19,314/70 yamepatiwa maelezo ya kuridhisha.

**318.** *Ukodishaji wa Gari la Binafsi Ileje (Sh. 123,887/70)—Aya ya 368:—*

(a) Afisa anayehusika amekatwa asilimia 10 ya mshahara wake wa mwezi mmoja.

(b) Vifaa vyote vimethibitika kupokelewa na kuingizwa daftarini. Maelezo kuhusu idadi ya vifaa hivyo, uzito wake na magari yaliyofanya kazi ya uchunguzi yaliyowasilishwa Ukaguzi.

(c) Kiasi cha Sh. 9,017/80 kilicholipwa zaidi kimerejeshwa na mhusika, na hoja inayohusika imejibiwa na kufungwa.

**319.** *Mfuko wa Kuhudumia Magari (Plant and Transport Maintenance Fund)—Aya ya 369:—*

Hesabu za mfuko huo zilitayarishwa na kuwasilishwa Ukaguzi.

**320.** *Regional Development Fund—Aya ya 370:—*

Mkoa umeeleza kuwa hesabu hizo zimekwisha hakikiwa na Ukaguzi.

**321.** *Matokeo ya Kaguzi Hesabu za Ofisi za Kurugenzi—Aya ya 371:—*

(a) Wizi huo bado unachunguzwa na Polisi.

(b) Mkoa umetayarisha taarifa ya upotevu baada ya kushindwa kupata maelezo ya kuridhisha toka kwa mhusika kuhusu upokeaji na matumizi ya radio hizo.

(c) I (i) Maelezo kuhusu kiasi kilichokusanywa yaliyowasilishwa Ukaguzi.

(ii) Uthibitisho wa kupokelewa fedha hizo na kuwekwa kwenye mfuko wa Serikali ulitolewa Ukaguzi.

(iii) Maelezo kuhusu fedha hizo yaliwasilishwa Ukaguzi.

II (i) Uthibitisho wa Sh. 33,421/10 kupelekwa benki ulitolewa kwa Wakaguzi, na hoja inayohusika ilijibiwa na kufungwa.

III (ii) Mchanganuo wa Masurufu kwa mwaka 1980/81 na 1981/82 imetayarishwa na kuwasilishwa Ukaguzi. Kuhusu Mchanganuo kwa mwaka 1979/80 Mkoa umeeleza kuwa imeshindikana kutengeneza mchanganuo huo kutokana na ukosefu wa karatasi.

IV Maelezo ya kuridhisha kuhusu vifaa hivyo yaliwasilishwa Ukaguzi.

(d) (i) Vifaa vya thamani ya Sh. 138,005/- vimethibitika kupokelewa na maelezo kuhusu matumizi yake yaliwasilishwa Ukaguzi.
(ii) Saruji ya thamani ya Sh. 29,570/- bado kupokelewa toka RTC.
(iii) Magizo ya Kamati yamezingatiwa.
(iv) Hakuna maoni.
(vii) na (viii) Maonyo ya Kamati yamezingatiwa.
(e) (i) Maelezo kuhusu vifaa vya thamani ya Sh. 1,640,840/50 yaliwasilishwa Ukaguzi.
(f) (i) Maelezo ya kuridhisha kuhusu matumizi ya Saruji ya thamani ya Sh. 3,688/80 yalitolewa Ukaguzi.
(iv) Vifaa vyote vilivyokuwa vimeazimwa vimerejeshwa na Mkoa umeithibitishia Hazina kuwa mtindo huo wa kukopeshana mali ya Serikali bila kufuata utaratibu uliowekwa umeachwa.
(v) Agizo la Kamati limezingatiwa.
(g) (i) Mkoa umezingatia maoni ya Kamati.
(ii) Mpaka sasa uchunguzi wa Polisi haujakamilika kuhusu suala hilo.
(iii) Maoni ya Kamati yamezingatiwa.
(iv) Fidia hiyo haijalipwa na mhusika.
(v) Mkoa umeeleza kuwa vifaa vyote vilivyohojiwa vimethibika kupokelewa.
(h) (iii) Agizo la Kamati limezingatiwa.

322. *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 372:—*
Mkoa umeyazingatia maagizo ya Kamati.

## FUNGU 79.—MKOA WA MOROGORO

323. *Masuali ya Ukaguzi—Aya ya 373:—*
Kati ya maswali 339 yaliyokuwa yamesalia, maswali 85 yamejibiwa na kufungwa, bado 254.

324. *Matokeo ya Hesabu—Aya ya 374:—*
Tofauti zilizokuwepo kati ya Mkoa na Ukaguzi kuhusu hesabu ya matumizi zaidi na deni la benki zimerekebishwa, na hatua za kuhalalisha matumizi yaliyofanyika zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa na Bunge zimechukuliwa.

325. *Usuluhisho wa Hesabu ya Benki na Shahada ya Usahihi—Aya ya 375:—*
Hakuna maoni zaidi.

326. *Masurufu na Karadha zinazodaiwa—Aya ya 376:—*
(a) (i) Mkoa umechukua hatua za kuepuka makosa hayo siku zijazo.
(iv) Hakuna maoni.
(b) Hoja inayohusika imejibiwa

327. *Malipo Yasiyo Kawaida na au yenye Shaka—Aya ya 378:—*
(a) Kati ya kiasi cha Sh. 71,105/85 kilichokuwa kimesalia, kiasi cha Sh. 57,916/40 kimepatiwa maelezo ya kuridhisha, bado kiasi cha Sh. 13,189/75.
(c) Suala hilo bado halijapatiwa usuluhisho.

**328.** *Ulegevu wa Dhibiti Katika Ununuzi wa Vifaa na Uwekaji Hesabu wake—Aya ya 379:—*

(a) Vifaa vya thamani ya Sh. 101,703/65 zimethibitishwa kupokelewa, bado vifaa vya thamani ya Sh. 304,808/10.

(c) Mhusika alishtakiwa kwa kuhusika na wizi wa vifaa hivyo na kesi yake bado ipo Mahakamani.

**329.** (a) *Nunuzi juu ya Kiwango—(Sh. 853,009/90)—Aya ya 380:—* Agizo la Kamati linafuatwa.

(b) Mkoa umechukua hatua za kuwaelemisha Warranti Holder kuhusu utaratibu unaopasa kufuatwa wakati wa kufanya manunuzi.

**330.** *Utovu katika Dhibiti ya Ukusanyaji wa Maduhuli na Uwasilishaji wa Maduhuli ya Serikali Benki—Aya ya 381:—*

(a) Suala hili limeshughulikiwa kama ifuatavyo:—

(i) Taarifa ya upotevu wa Sh. 6,542/90 imetayarishwa na kuwasilishwa Hazina.

(ii) Hazina haina maoni zaidi kuhusu kiasi cha Sh. 3,797/- ambacho kinaendelea kukatwa toka kwenye mshahara wa mhusika.

(iii) Nyaraka za thamani ya Sh. 29,982/95 bado kupatikana.

(iv) Kuhusu potevu zinazohusu Ofisi za RADO na Mifugo, Morogoro Hazina haina maoni zaidi kuhusu vipengele hivyo.

(b) Matokeo ya utafutaji wa vitabu hivyo ni kama ifuatavyo:—

(i) Birth Certificates—Vitabu vyote 6 bado kupatikana.
U.P.E. Books Mkoa umeeleza kuwa vitabu vilivyokuwa vinakosekana ni 19, na vyote hivyo vimepatikana.
ERV. BOOKS—Kitabu hicho kipo Mahakamani.
(Mifugo Mahenge).
ERV Books—Kiasi cha Sh. 4,252/- (Kilimo Mahenge) kemethibitishwa kupokelewa Benki.
Fishing Books—Vitabu vimepatikana 2 (form 2)
(form 6)—Vitabu 5 vimepatikana.
Farm Produce—vitabu vyote bado kupatikana.
ERV. Books—Vitabu vyote bado kupatikana.
(Kilimo Morogoro).

(c) Kiasi cha Sh. 174,818/45 kimekusanywa.

(d) Fedha hizo bado kukusanywa.

**331.** *Potevu za Fedha na Vifaa—Aya ya 383:—*

(a) (i) Kesi imefungwa kwa sababu mhusika ametoroka.
(ii) Hukumu bado kutolewa na Mahakama.
(iii) Polisi bado wanaendelea na upelelezi.
(iv) Maelezo kuhusu potevu hizo yalitolewa Ukaguzi.

(b) (i) Upelelezi wa Polisi kuhusu upotevu huu unaendelea.
(ii) Juhudi za kuwapata wahusika ili watie saini kwenye hati za kutolea mafuta zimeshindikana na Mkoa umeamua kuandika taarifa ya upotevu kuhusu suala hilo.

(iii) Mhusika na upotevu huo ameacha kazi, na upelelezi wa Po isi kuhusu suala hilo unaendelea.

(iv) Mkoa haukutoa maelezo kuhusu kipengele hicho.

332. *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 384:—*

(a) (ii) Hati za thamani ya Sh. 227,717/- zimetiwa saini na wahusika kuthibitisha upokeaji wa vifaa hivyo.

(v) Madeni ya thamani ya Sh. 13,322/- yamekusanywa.

(vi) Madawa ya thamani ya Sh. 994,897/- yamethibitika kupokelewa na Ukaguzi imepatiwa uthibitisho huo.

(b) (iii) Vifaa vya thamani ya Sh. 120,912/- vimethibitika kupokelewa.

(iv) Hati za thamani ya Sh. 1,172,746/30 zimetiwa saini na wahusika kuthibitisha upokeaji wa vifaa hivyo.

(v) Hati za kuthibitisha kutolewa vifaa vya thamani ya Sh. 816,015/25 zimetiwa saini na wapokeaji wanaohusika.

(vii) Mkoa haukutoa maelezo kuhusu kipengele hicho.

(viii) Fedha hizo bado hazijarejeshwa na Mzabuni.

(x) Kati ya mauzo ya Sh. 56,341/- Mkoa umepokea 5,458/40. Na kuhusu upotevu wa mbegu za thamani ya Sh. 5,112/- mhusika ameshtakiwa Mahakamani kwa wizi wa vifaa hivyo. ...

(c) (ii) Mhusika alishtakiwa kwa upotevu huo, lakini Mahakama ilimwachia huru kwa sababu ya kukosekana ushahidi wa kutosha.

(iv) Mbuzi 50 waliokuwa wanakosekana sasa wamepatikana.

(v) Kiasi cha Sh. 120/- kimekusanywa.

## FUNGU 80.—MKOA WA MTWARA

333. *Taahira Kuletwa Hesabu—Aya ya 385:—*

Maagizo ya Kamati yamezingatiwa.

334. *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 386:—*

Kati ya maswali 231 yaliyosalia, maswali 34 yamejibiwa na kufungwa, bado maswali 197 ambayo Mkoa unaendelea kuyashughulikia.

335. *Matokeo ya Hesabu—Aya ya 387:—*

Suala hilo bado kupatiwa ufumbuzi.

336. *Usuluhisho wa Hesabu ya Benki na Shahada ya Usahihi—Aya ya 388:—*

Mkoa umeeleza kuwa hesabu za maduhuli kuhusu Ofisi ya Mkoa na Mtwara Vijijini, zimesuluhishwa hadi kufikia tarehe 30/6/81. Wilaya ya Newala na Masasi hazihusiki kwa vile fedha za maduhuli walizokuwa wakikusanya zilikuwa zinaingizwa katika akaunti ya "Recurent Expenditue" ambayo imekwishafanyiwa usuluhisho hadi 30/6/81. Mfuko wa kuhudumia magari ulisuluhishwa hadi kufikia 30/6/81.

**337.** *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka na Yenye Hati Pungufu—(Sh. 10,184,858/35)—Aya ya 389:—*

Kati ya maswali 16 ya thamani ya Sh. 494,016/65 yaliyokuwa yamesalia, maswali 13 ya thamani ya Sh. 339,776/65 yamejibiwa na kufungwa. Juhudi ya kujibu maswali 3 yaliyosalia zinaendelea.

**338.** *Karadha na Masurufu—Karadha za Binafsi—(Sh. 2,203,899/70) na Masurufu Sh. 603,044/45—Aya ya 390:—*

Mchanganuo kuhusu Karadha za binafsi ulitayarishwa na kuwasilishwa Ukaguzi, na Mkoa umezingatia umuhimu wa michanganuo hiyo kutengenezwa na kuwasilishwa mapema Ukaguzi siku zijazo. Na yale masurufu ya Sh. 800/- yaliyokuwa yamesalia kurejeshwa sasa yemarejeshwa.

**339.** *Vifaa Vilivyolipiwa vimepokelewa kwa Pungufu—(Sh. 73,299/10)—Aya ya 391:—*

Vifaa vya thamani ya Sh. 1,456/10 vimethibitika kupokelewa na kuingizwa daftarini.

**340.** *Dosari Katika Uwekaji wa Hesabu za Vifaa—Aya ya 392:—*

(a) Kutokana na ukosefu wa kumbukumbu Mkoa umeshindwa kutoa uthibitisho wa upokeaji wa vifaa hivyo.

(b) Mkoa ulifanya mchanganuo na kupata hesabu ya mbao wanazozihitaji kwa miradi yao. Mbao zilizozidi zimeuzwa kwa Idara nyingine.

(c) Vifaa vya thamani ya Sh. 720,683/70 vimethibitika kupokelewa na kuingizwa madaftarini na juhudi ya kutafuta vifaa vilivyosalia zinaendelea. Pia, Mkoa umeithibitishia Hazina kuwa, kila mradi sasa umefunguliwa Leja.

**341.** *Ulegevu Katika Kukusanya Maduhuli ya Serikali—Aya ya 393:—*

Kiasi cha Sh. 14,710/70 kimekusanywa kati ya Sh. 24,746/70 zilizokuwa zinadaiwa, na juhudi ya kukusanya kiasi kilichosalia zinaendelea.

**342.** *Ruzuku kutoka mfuko wa Maendeleo ya Mkoa—(Sh. 85,000/-)—Aya ya 394:—*

Mkoa umeeleza kuwa Sh. 85,000/- zililipwa kutoka kwenye kifungu cha mradi wa maji na si kutoka mfuko wa RDF kama ilivyoelezwa katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Maelezo ya kuridhisha kuhusu matumizi ya fedha hizo yaliwasilishwa Ukaguzi.

**343.** *Tuhuma ya wizi wa Fedha na Vifaa—Aya ya 395:—*

Uchunguzi uliofanyika umeonyesha kuwa mifuko 516 ya saruji ilitumika kujengea jengo la ufundi la SIDO, ghala moja na visima viwili katika eneo la Nachitura, Newala na Idara ya Ujenzi imethibitisha usahihi wa matumizi hayo.

**344.** *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 396:—*

(a) (ii) Hakuna maoni.

(iii) Mkoa umethibitisha kuwa vifaa vyote vilipokelewa.

(b) (i) Vifaa vyote vilivyoazimwa vimerejeshwa.

(ii) Vifaa vyote vilipokelewa.

(c) (i) Vifaa vyote vimethibitika kupokelewa.

(ii) Maelezo kuhusu matumizi ya vifaa hivyo yalitolewa Uhakikimali.

(iii) Hadi sasa kiasi hicho hakijakusanywa.

(iv) Mkoa umeeleza kuwa kutokana na hati ya madai ya Sh. 28,800/- kuhesabiwa mara mbili kiasi sahihi kinachodaiwa ni Sh. 116,152/30 badala ya Sh. 144,952/50. Kati ya kiasi hicho (Sh. 116,152/30), Sh. 17,313/05 zimekusanywa, ng'ombe wa thamani ya Sh. 60,800/- walitolewa kwa askari wagombea uhuru, na Sh. 38,039/25 zimesalia kukusanywa.

(d) Mkoa umekwishapokea Fomu SF 7 ambazo wanazitumia hivi sasa kwa kutolea vifaa.

(i) Uthibitisho huo ulitolewa Uhakikimali.

(e) (i) Taarifa ya Upotevu ilitayarishwa na kuwasilishwa Uhakikimali.

(ii) Maelezo kuhusu mbegu hizo yalitolewa Uhakikimali.

(f) (i) Vifaa vya thamani ya Sh. 10,380/- havijathibitika kupokelewa na kuingizwa vitabuni.

(ii) Mkoa haukutoa maelezo ya kuridhisha kuhusu kipengere hiki.

(iii) Mabati 210 bado kupatikana.

(g) Maelezo kuhusu mauzo ya madawa hayo yalitolewa uhakikimali.

## FUNGU 81.—MKOA WA MWANZA

345. *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 397:—*

Kati ya maswali 101 yaliyokuwa yamesalia maswali 50 yamejibiwa na kubakiza 51 ambayo yanaendelea kushughulikiwa.

346. *Orodha za Hesabu Hazikuletwa—Aya ya 398:—*

(iii) Kasoro zilizokuwa zimeonekana katika hesabu ya mfuko wa magari zimerekebishwa.

347. *Matokeo ya Hesabu—Aya ya 399:—*

Maagizo ya Kamati yamezingatiwa.

348. *Usuluhisho wa Hesabu ya Benki na Shahada ya Usahihi—Aya ya 400:—*

Maswali yote mawili yaliyokuwa yanahoji dosari zilizobainika katika usuluhisho wa benki yamejibiwa na kufungwa.

349. *Karadha na Masurufu—Aya ya 401:—*

Mkoa haujatoa hesabu ya kiasi cha karadha na masurufu kilichokusanywa hadi sasa.

350. *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka na yenye Hati Pungufu—Aya ya 402:—*

(i) Utaratibu sahihi utafuatwa siku zijazo.

(ii) Jitihada ya kutafuta nyaraka zilizosalia zinaendelea ili kusuluhisha suala hilo.

(iii) Mkoa umetakiwa kutafuta nyaraka zote zilizosalia na kuzipata.

**351.** *Orodha ya Hesabu ya Mali na Dhima—Aya ya 404:—*
Ufumbuzi wa Hazina bado kupatikana kuhusu suala hilo.

**352.** *Nunuzi Mitaani—(Sh. 3,797,813/95)—Aya ya 405:—*
Hazina haina maoni zaidi kuhusu aya hizo.

**353.** *Malipo Zaidi—(Sh. 121,800/75)—Aya ya 406:—*
Hazina haina maoni zaidi kuhusu aya hizo.

**354.** *Mishahara—(Sh.14,140/50)—Aya ya 407:—*
Kiasi cha Sh. 10,095/25 kimerejeshwa, na juhudi za kupata kiasi kilichosalia zinaendelea.

**355.** *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 409:—*

(a) Kifungu hiki bado hakijashughulikiwa.

(b) (i) Upelelezi wa Polisi kuhusu upotevu wa vifaa vya thamani ya Sh. 14,678/- na upotevu wa W.C. Pan ya thamani ya Sh 7,000/- ulikamilika, lakini wahusika waliachiliwa huru kwa sababu ya kukosekana ushahidi wa kutosha. Hata hivyo kutokana na uzembe wao watuhumiwa hao wote walifukuzwa kazi na Mkoa kama hatua ya nidhamu kufuatana na Civil Service Regulations.

(ii) Mtuhumiwa ameshindikana kupatikana na Mkoa umeamua kufuta upotevu huo.

(iii) Kesi inayohusu upotevu wa Sh. 11,327/- imefutwa kutokana na kukosekana ushahidi wa kutosha.

Kuhusu upotevu wa vifaa vya thamani ya Sh. 6,800/-, kesi hii pia imefutwa kwa sababu ya kukosekana ushahidi wa kutosha. Hata hivyo kwa sababu ya uzembe huo mhusika amefukuzwa kazi.

(iv) Suala hili lilifungwa kutokana na kukosekana ushahidi wa kutosha. Hata hivyo Afisa Mifugo wa Wilaya ya Ukerewe na mlinzi anayehusika wote kwa pamoja wamelipishwa Sh. 4,500/- kufidia upotevu huo.

(v) Hakuna maoni.

(c) Kifungu hicho bado kushughulikiwa inavyotakiwa.

## FUNGU 82.—MKOA WA RUVUMA

**356.** *Taahira Kuletwa Hesabu—Aya ya 410:—*
Utayarishaji wa hesabu unaendelea kuathiriwa na mashine ya hesabu ambayo huharibika mara kwa mara. Kwa sababu ya kukosekana mashine mpya za kununua Mkoa umeshauriwa kuandika hesabu zake kwa mkono kufuatana na Waraka wa Uhasibu Na. 1 wa 1980, na pia kutumia mashine ya akiba iliyopo Mkoani Mbeya, na maagizo hayo yanafuatwa.

**357.** *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 411:—*
Kati ya maswali 770 yaliyokuwa yamesalia, maswali 273 yamejibiwa na kufungwa, bado 497 ambayo yanaendelea kushughulikiwa.

Mkoa haujatoa maelezo kuhusu zile ripoti maalum 4 ambazo zilikuwa hazijajibiwa. Hazina inaendelea kufuatilia suala hilo.

358. *Matumizi Zaidi—Aya ya 412:—*

Matumizi hayo yameombewa uhalalisho wa Bunge. Na kuhusu usuluhishaji wa hesabu za benki, agizo la Kamati halijatekelezwa kikamilifu.

359. *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka—(Sh. 70,927/55) na yenye Hati Pungufu—Sh. 5,634,285/65—Aya ya 414:—*

Nyaraka za thamani ya Sh. 70,927/55 bado kupatikana. Na kati ya kiasi cha Sh. 4,653,734/60 kuhusu matumizi yenye hati pungufu, hati za thamani ya Sh. 383,396/45 zimepatikana. Juhudi zinaendelea za kutafuta nyaraka zinazokosekana.

360. *Karadha Zinazodaiwa, Masurufu Yasiyorejeshwa—Aya ya 415:—*

Mkoa umeshindwa kutoa michanganuo ya Karadha na masurufu yanayodaiwa kwa kisingizio kuwa nyaraka na kumbukumbu zinazohusika hazionekani. Mkoa umetakiwa kuendelea kutafuta nyaraka hizo ukizingatia kuwa huo ndiyo msingi wa kuuwezesha kufuatilia madeni hayo na kuyakusanya.

361. *Utovu wa Dhibiti Katika Ulipaji wa Mishahara na Posho—Aya ya 416:—*

(a) Fedha hizo bado kurejeshwa na mhusika na juhudi ya kuzipata zinaendelea.

(b) Mhusika anaendelea kukatwa Sh. 300/- kila mwezi na hadi mwezi Julai, 1984 amekwisha katwa Sh. 6,300/-.

(c) Fedha hizo bado kurejeshwa.

362. *Utovu wa Dhibiti Katika Ulipaji wa Madai ya Karadha na Mikopo—Aya ya 417:—*

(a) Wahusika wanaendelea kukatwa fedha hizo toka mishahara yao. Mkoa haukuonyesha kiasi kilichokusanywa hadi sasa.

(c) Kati ya kiasi cha Sh. 81,243/20 kilichokuwa kinadaiwa kiasi cha Sh. 22,081/40 kimekusanywa.

(d) Maagizo ya Kamati yametekelezwa.

363. *Malipo Yasiyo ya Kawaida na/au yenye Mashaka—Aya ya 418:—*

(a) Mkoa umethibitisha kuwa bidhaa za thamani ya Sh. 136,213/- zimepokelewa.

(e) Tatizo hilo bado halijapatiwa ufumbuzi, matumizi yaliyofanywa zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa katika bajeti yameombewa uhalalisho wa Bunge.

(f) Maelezo ya kuridhisha kuhusu fidia hiyo yalitolewa Ukaguzi.

364. *Nunuzi Zisizo Kabidhi zimesababisha Gharama Ziada kwa Serikali—(Sh. 352,900/-)—Aya ya 419:—*

Maelezo kuhusu nunuzi hizo yaliwasilishwa Ukaguzi, na Mkoa umeithitishia Hazina kuwa manunuzi yote utakayofanya siku zijazo yatafuata utaratibu uliowekwa chini ya kanuni za fedha.

365. *Vifaa Havikuingizwa Madaftarini—(Sh. 3,779,604/-)—Aya ya 420:—*

Mkoa umethibitisha kupokelewa kwa vifaa vya thamani ya Sh. 576,870/20 na kuingizwa daftarini.

366. *Potevu ya Fedha na Vifaa—Aya ya 421:—*

(a) (i) Hadi sasa kesi hiyo bado iko Mahakamani.

(iii) Mtuhumiwa alifungwa jela miaka 3 na kuamriwa kuifidia Serikali upotevu huo. Mkoa unafuatilia suala hilo ili kuhakikisha kuwa fedha hizo zinarejeshwa.

(iv) Watumishi waliohusika wamefukuzwa kazi.

(v) Kesi hiyo bado haijasikilizwa.

(b) Kesi hiyo bado ipo chini ya upelelezi wa Polisi.

367. *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 422:—*

(a) Regional Veterinary Office, Songea.

(i) Mkoa umethibitisha kupokelewa kwa Ng'ombe 17 wenye thamani ya Sh. 25,500/- na kuingizwa daftarini.

(ii) Agizo la Kamati limetekelezwa kikamilifu.

(iv) Kati ya madawa ya thamani ya Sh. 128,015/20 yaliyosalia, madawa ya thamani ya Sh. 35,428/30 yameuzwa na fedha hizo zimepatikana, madawa ya thamani ya Sh. 14,627/50 hayafai kutumika kwa sababu muda wake umekwisha, bado madawa ya thamani ya Sh. 113,387/70 ambayo yanangojea kuuzwa.

(b) (i) Suala hilo bado lipo chini ya upelelezi wa Polisi.

(ii) Uthibitisho wa kupokelewa madawa yenye thamani ya Sh. 77,414/- umetolewa Uhakikimali.

## FUNGU 83.—MKOA WA SHINYANGA

368. *Taahira kuletwa Hesabu—Aya ya 423:—*

(i)—(iii) Hesabu hizo zilitayarishwa na kuwasilishwa Ukaguzi.

369. *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 424:—*

Kati ya maswali 362 yaliyosalia, maswali 230 yamejibiwa na kufungwa. Bado maswali 132 ambayo Mkoa unaendelea kuyashughulikia.

370. *Matokeo ya Hesabu—Aya ya 425:—*

(a) Hazina pia haikuridhishwa na maelezo yaliyotolewa kuhusu matumizi hayo. Imekuwa tabia ya Mkoa huu kutumia fedha zaidi kila mwaka na kusingizia maamuzi ya kisiasa kuwa ndiyo yanayosababisha hali hiyo itokee kwa vile hawawezi kuyapinga. Ukweli ni kwamba Mkoa umekuwa mlegevu katika kudhibiti matumizi yake kwa sababu haufuati kanuni za fedha. Mkoa umeonywa kuacha tabia hiyo. Matokeo ya onyo hilo yatizamwe katika miaka inayofuata kuanzia 1982/83.

Kati ya kiasi cha Sh. 7,538,224/70 ambacho Halmashauri ya Mji wa Shinyanga ilikuwa ikidaiwa na Mkoa, Sh. 818,235/40 zimerejeshwa na kubakia Sh. 6,719,989/30 ambazo Mkoa unaendelea na juhudi ya kuzipata toka kwa Halmashauri hiyo.

(b) Maagizo ya Kamati yamezingatiwa.

371. *Usuluhisho wa Hesabu ya Benki na Shahada ya Usahihi—Aya ya 426:—*

Suluhisho za hesabu za benki kwa matumizi ya Kawaida na Maduhuli zilitengenezwa na kuwasilishwa Ukaguzi.

372. *Karadha na Masurufu—Aya ya 427:—*

Hazina haina maoni juu ya suala hili.

373. *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka na Yenye Hati Pungufu—Aya ya 428:—*

Kati ya matumizi yasiyo na nyaraka ya thamani ya Sh. 140,295/25 yaliyohojiwa, nyaraka za thamani ya Sh. 92,090/55 zimepatikana na kubakiza nyaraka za thamani ya Sh. 48,204/70. Na kati ya matumizi yenye nyaraka pungufu ya thamani ya Sh. 717,484/20, matumizi ya thamani ya Sh. 402,958/55 yamepatiwa maelezo ya kuridhisha. Na kuhusu maswali ya Ukaguzi 51 yanayohoji malipo kwa ankara vifani ya thamani ya Sh. 3,235,618/05, maswali 35 ya thamani ya Sh. 2,231,323/25 yamejibiwa na kufungwa, bado maswali 16 ya thamani ya Sh. 1,004,294/80 ambayo Mkoa unaendelea kuyashughulikia.

374. *Matumizi ya Batili—Aya ya 429:—*

Hoja zote 3 za thamani ya Sh. 37,303/20 ambazo zilisalia zilijibiwa na kufungwa.

375. *Ununuzi Mitaani—Aya ya 430:—*

Kati ya maswali 37 yaliyosalia yenye thamani ya Sh. 1,738,798/70, maswali 13 yenye thamani ya Sh. 486,314/75 yamejibiwa na kufungwa, bado maswali 24 ya thamani ya Sh. 1,282,483/95 ambayo Mkoa unaendelea kuyashughulikia.

Mkoa umeahidi kufuata utaratibu utakapolazimika tena kufanya manunuzi mitaani.

376. *Malipo Kuepa Muda wa Matumizi—Aya ya 431:—*

Maelezo ya kuridhisha kuhusu matumizi ya fedha hizo yaliwasilishwa Ukaguzi.

377. *Utovu wa Dhibiti ya Vifaa—Aya ya 432:—*

(a) (i) Agizo la Kamati limezingatiwa.

(ii) Vifaa vya thamani ya Sh. 5,236/- vilipokelewa na kuingizwa katika vitabu vya Mwanhuzi Health Centre.

(iii) Kuni za thamani ya Sh. 7,500/- zilinunuliwa na kupokelewa na Mkuu wa Wilaya ya Maswa kwa matumizi ya Nyumbani kwake kama Mkuu wa Wilaya.

(iv) Hakuna Maoni.

(vi) Vifaa vya thamani ya Sh. 4,680/- visivyopokelewa vimetolewa taarifa ya upotevu.

(vii) Vifaa vya thamani ya Sh. 67,243/45 vimepokelewa kati ya vifaa vya thamani ya Sh. 85,243/45 vilivyohojiwa.

(viii) Hakuna Maoni.

(ix) Wahusika wamekatwa mishahara yao kufidia upotevu huo.

(x) Vifaa vya thamani ya Sh. 5,148/15 vimethibitika kupokelewa.

(xi) Onyo la Kamati limezingatiwa.

(xii) Hakuna Maoni.

(b) (ii) Vifaa vya thamani ya Sh. 30,048 vimethibitishwa kupokelewa.

(iii) Vifaa vya thamani ya Sh. 8,000/- vilitolewa maelezo Ukaguzi.

(c) Maelezo kuhusu mafuta ya thamani ya Sh. 1,982,787/55 yalitolewa Ukaguzi.

(d) Mhusika na upotevu wa Sh. 2,750/80 alishtakiwa kwa wizi wa vifaa hivyo na kufungwa miaka mitatu.

378. *Potevu ya Fedha—Aya ya 433:—*

Hazina haina maoni juu ya suala hili.

379. *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 434:—*

(i) (v) Hati za thamani ya Sh. 6,201/40 zilipatikana na kuwasilishwa Uhakikimali.

(vi) Mkoa umefuta madawa ya thamani ya Sh. 11,949/-, na unangojea kibali cha Hazina kufuta madawa ya thamani ya Sh. 11,025/-.

(vii) Madawa ya thamani ya Sh. 374,922/20 yamethibitika kupokelewa.

(ix) Mkoa ulitoa mchanganuo wa jinsi madawa hayo yalivyogawanywa kwa Wilaya mbalimbali. Pia umeeleza utaratibu wa uwasilishaji wa fedha zinazopatikana kutokana na mauzo ya madawa hayo.

(b) (i) Sula hili bado limo mikononi mwa Mahakama.

(ii) Mkoa unafuatia ufidiaji ama ufutaji wa hasara hiyo.

(iii) Watumishi waliohusika wamefidia mbao za thamani ya Sh. 4,417.20, na Mkoa umeomba kibali cha Hazina kufuta mbao za thamani ya Sh. 17,668/80. Wahusika na upotevu wa 'alternator ya thamani ya Sh. 5,378/- wametakiwa kufidia hasara hiyo kwa kukatwa Sh. 100/- kila mwezi. Hadi June 1983 walikwishakatwa Sh. 3,000/-.

(iv) Kiasi cha Sh. 1,501/35 kimekwishakatwa kutoka kwa watumishi waliohusika na upotevu wa Sh. 5,045/85. Kuhusu upotevu wa Sh. 18,746/-, Afisa mhasibu amefuta mtama wa thamani ya Sh. 2,052/- kutokana na uwezo aliopewa chini ya GN. 210 ya 1971, na pia ameomba kibali cha Hazina kufuta hasara ya mifuko ya saruji yenye thamani ya Sh. 16,694/-.

(v) Taarifa hiyo bado inashughulikiwa na Hazina.

(vi) Suala hili pia bado linashughulikiwa na Hazina.

380. *Taahira ya Kuletwa Hesabu—Aya ya 435:—*

Agizo limezingatiwa.

(i) Halmashauri ya Mji wa Singida haijarejesha fedha hizo hadi sasa.

(ii) Hazina haina maoni juu ya suala hilo.

381. *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 436:—*

Kati ya maswali 294 yaliyosalia, maswali 140 yamejibiwa na kufungwa, na maswali 154 yaliyosalia yanaendelea kushughulikiwa.

382. *Matumizi Zaidi—Aya ya 437:—*

Mkoa umezingatia maagizo ya Kamati.

383. *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka na Yenye Hati Pungufu—Sh. 20,686,512/70—Aya ya 438:—*

Kati ya kiasi cha Sh. 12,029,302/45 kilichokuwa kimesalia, nyaraka za thamani ya Sh. 2,556,246/35 zimepatikana na kubakiza nyaraka za thamani ya Sh. 9,473,056/10 ambazo zinaendelea kutafutwa.

384. *Matumizi Batili—(Sh. 73,581/75)—Aya ya 439:—*

Mkoa umeahidi kuwa matumizi ya aina hiyo hayatokea tena.

385. *Ulegevu Katika Dhibiti ya Ulipaji Mishahara naUjira wa Vibarua—(Sh. 730,802/90)—Aya ya 440:—*

(i)—(ix) Hadi sasa kiasi cha Sh. 169,514/20 kimerejeshwa, na juhudi za kupata kiasi kilichosalia zinaendelea. Hata hivyo, kati ya watumishi wanaodaiwa kuna baadhi yao wamefariki na wengine hawajulikani mahali walipo. Kutokana na hali hiyo kuna wasiwasi kuwa huenda kiasi kilichosalia kisirejeshwe kikamilifu.

386. *Ulegevu Katika Dhibiti ya Ununuzi na Vifaa na Uwekaji Hesabu wake—Aya ya 441:—*

(a) Vifaa vya thamani ya Sh. 1,133,523/- vimethibitika kupokelewa na kuingizwa daftarini, vifaa vya thamani ya Sh. 98,185/40 vimepotea na kuandikiwa taarifa ya upotevu na vifaa vilivyosalia vya thamani ya Sh. 524,577/30 vinaendelea kutafutwa.

(b) Hadi sasa madawati 226 ya thamani ya Sh. 73,935/90 bado kupokelewa toka SIDO Singida.

(c) Mkoa unaendelea kuwasiliana na Hazina ili kuhalalisha manunuzi hayo. Hadi sasa manunuzi ya thamani ya Sh. 379,575/- yamekwishahalalishwa.

387. *Mambo Yenye Mashaka—Aya ya 442:—*

(a) Mkoa umezingatia onyo la Kamati.

(b) (i) Mkoa unawasiliana na Wazo Hill Dar es Salaam ili kurejeshewa thamani ya Saruji hiyo.

(ii) Marekebisho yalifanyika, na hoja inayohusika imejibiwa na kufungwa.

389. *Malimbikizo ya Appropriation-in-aid* (*Sh. 722,494/60*)—*Aya ya 443*:—

Jitihada za kutayarisha michanganuo hiyo pamoja na kukusanya malimbikizo zinaendelea.

390. *Utengenezaji wa Magari na Mashine—Aya ya 444*:—

(i) Maagizo ya Kamati yamezingatiwa.

(ii) Hakuna maoni.

391. *Malipo ya Wizi*—(*Sh. 311,750/-*)—*Aya ya 445*:—

(a) Hakuna Maoni.

(b) Mkoa umeridhika kuwa vifaa hivyo vimepotea na taarifa ya upotevu imekwishatayarishwa na kuwasilishwa Hazina.

392. *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 446*:—

(a) (i) Wahusika wanakatwa mishahara yao kufidia thamani ya vifaa ambavyo wameshindwa kuvirejesha.

(ii) Vifaa vyote vya thamani ya Sh. 1,694/50 vimepatikana.

(iii) Vifaa vya thamani ya Sh. 191,240/- havijapokelewa.

(iv) Maelezo kamili yatatolewa baada ya Polisi kukamilisha upelelezi wao kuhusu upotevu huo.

(b) Mkoa bado unaendelea kutayarisha mchanganuo huo.

## FUNGU 85.—MKOA WA TABORA

393. *Hesabu za mwaka 1979/80—Aya ya 447*:—

(a) Mkoa umeithibitishia Hazina kuwa onyo la Kamati limezingatiwa. Matokeo yatizamwe katika miaka inayofuata.

(b) Matumizi hayo yameonyeshwa katika tanbihi ya hesabu za mwaka wa fedha 1982/83 kama Kamati ilivyoagiza.

(c) Hadi sasa kiasi cha Sh. 4,127/50 kuhusu karadha na Sh. 218,287/10 kuhusu masurufu kimebakia kukusanywa. Suala la 'Ledger Cards 691—10 na 691—20 pamoja na bakaa zake limeshughulikiwa kama Kamati ilivyoagiza.

(d) Mkoa haukupata shahada ya usahihi katika mwaka wa fedha 1981/82. Jitihada za kutimiza lengo hilo zinaendela.

394. *Hesabu za mwaka 1980/81—Aya ya 448*:—

(a) (i) Orodha hiyo ilitayarishwa na kuwasilishwa Ukaguzi.

(ii) Mkoa haukutayarisha hesabu hizo kwa dai kuwa Kamati iliwaagiza kutayarishwa hesabu hizo upya kuanzia tarehe 1.7.83. Mkoa utawajibika kutayarisha hesabu zote za miaka ya nyuma mpaka msamaha wa kutotayarisha hesabu hizo utolewe na Hazina.

(iii) Usuluhisho wa hesabu hizo bado kufanyika.

(iv) Kiasi cha Sh. 23,552/- kuhusu karadha kimekusanywa bado Sh. 27,864/- ambazo juhudi ya kuzikusanya zinaendelea. Ukaguzi bado haijakamilisha uhakiki wa hesabu ya masurufu; na kanuni ya urejeshaji masurufu pamoja na tozo ya asilimia 10 inatekelezwa.

(b) (i) Onyo la Kamati limezingatiwa. Matokeo yatizamwe katika miaka inayofuata.

(ii) Maagizo hayo yametekelezwa na Mkoa.

395. *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 449:—*

Kati ya maswali 145 yaliyokuwa hayajajibiwa, maswali 29 yamejibiwa na kufungwa, bado 116 ambayo yanaendelea kushughulikiwa.

396. *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka na Yenye Hati Pungufu—(Sh. 992,554/90)—Aya ya 450:—*

(a) Hazina haina maoni juu ya suala hilo

(b) Maagizo ya Kamati yamezingatiwa.

397. *Utovu Katika Dhibiti ya Ulipaji Mishahara—Aya ya 451:—*

(a) Mmoja kati ya Watumishi watatu wanaodaiwa alirejea toka masomoni, na hadi sasa amekwisharejesha Sh. 2,500/- na makato toka kwenye mshahara wake yanaendelea. Wengine watalipishwa watakaporejea nchini.

(b) Kiasi cha Sh. 650/- kimerejeshwa na suala hilo sasa limefungwa.

398. *Ulegevu Katika Ununuzi wa Vifaa na Uwekaji Hesabu wake—Aya ya 452:—*

(a) Vifaa vyenye thamani ya Sh. 38,000/- bado kupatikana na suala hilo lipo Mahakamani.

(b) (i) Vifaa vyote vya thamani ya Sh. 51,570/- vimethibitika kupokelewa na kuingizwa katika daftari.

(ii) Mhusika ameshindwa kutoa Madawati hayo wala kufidia thamani yake, na suala hilo sasa limepelekwa Mahakamani. Matokeo ya hatua hiyo yasubiriwe.

(c) Hadi sasa vifaa hivyo havijapokelewa na Mkoa haujatamka hatua inayokusudia kuchukua kuhakikisha inavipata.

(d) Onyo la Kamati limezingatiwa.

(e) Jibu ni kama (d) hapo juu.

399. *Ulegevu katika Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali na Madai—Aya ya 453:—*

(a) (i) Kati ya Sh. 8,987/65 ambazo zilikuwa zimesalia kukusanywa ni kiasi cha Sh. 52/70 tu kilichokusanywa hadi sasa. Mkoa umeeleza kuwa uwezekano wa kukusanya kiasi zaidi ni mdogo sana kwa sababu wadaiwa wengi wamehama nchi na wengine wamefariki. Ikiwa itashindikana kupata kiasi hicho Mkoa utashauriwa kuleta Hazina maombi ya kukifuta kufuatana na kanuni za fedha.

(ii) Juhudi za kukusanya fedha hizo zinaendelea.

(iii) Mkoa umeeleza kuwa uwezekano wa kupatikana kiasi hicho ni mdogo sana. Kutokana na hali hiyo Mkoa utashauriwa kuchukua hatua za kukifuta kufuatana na kanuni za fedha

(iv) Mkoa umefanikiwa kukusanya kiasi cha Sh. 711,173/40 na juhudi za kukusanya kiasi kilichosalia zinaendelea.

(b) Kiasi cha Sh. 1,649,015/25 kimekusanywa kati ya kiasi cha Sh. 10,474,317/35 kilichokuwa kinadaiwa.

**400.** *Potevu za Fedha—(Sh. 102,704/70)—Aya ya 454:—*

(a) Juhudi za kumpata mtuhumiwa hazijafanikiwa.

(b) Suala hili bado linashughulikiwa na Polisi.

**401.** *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 455:—*

(a) Maelezo ya kuridhisha kuhusu upokeaji na matumizi ya vifaa hivyo yaliwasilishwa Uhakikimali.

(b) (i) Maelezo kuhusu upokeaji na matumizi ya vifaa vya thamani ya Sh. 107,979/- yaliwasilishwa Uhakikimali.

(ii) Mkoa umefanikiwa kukusanya Sh. 16,777/30 kati ya kias cha Sh. 34,340/10 kilichosalia.

(c) Mchanganuo huo ulitayarishwa na kuwasilishwa Uhakikimali. Kuhusu agizo la Kamati kuwa ledger za kuingizia na kutolea madawa zifunguliwe, Mkoa haukutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa agizo hilo. Idara ya Uhakikimali inafuatilia kuona kuwa agizo hilo linatekelezwa.

(d) Suala hilo linaendelea kushughulikiwa.

## FUNGU 86.—MKOA WA TANGA

**402.** *Taahira Kuletwa Hesabu—Aya ya 456:—*

Orodha ya mali na Dhima haijawasilishwa Ukaguzi.

Kuhusu hesabu ya Mfuko wa Plant and Maintenance, Mkoa umedai kuwa umeshindwa kutengeneza hesabu hiyo kwa vile hawakupewa mtaji (capital). Hazina haikubaliani na kisingizio hicho kwa vile hata bila mtaji inawezekana kutengeneza Mizania (Balance Sheet) na ikakubaliana. Hazina ilitoa Waraka Na. 3 wa 1975 kuelezea jinsi ya kutayarisha hesabu hizo na wengi waliofuata mwongozo huo wamefanikiwa kutengeneza hesabu hizo. Hata hivyo, suala zima la utunzaji wa mfuko huo pamoja na utayarishaji wa hesabu zake lilifanyiwa uchunguzi na Wizara ya Ujenzi ili kulipatia ufumbuzi kitaifa. Hazina ingali ikingojea matokeo ya uchunguzi huo.

**403.** *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 457.:—*

Kati ya maswali 168 yaliyosalia, maswali 96 yamejibiwa na kufungwa, na maswali 72 yamebakia.

**404.** *Matumizi Ziada—(Sh. 1,875,492/20)—Aya ya 458:—*

Agizo la Kamati limezingatiwa.

**405.** *Usuluhisho wa Hesabu ya Benki na Shahada ya Usahihi—Aya ya 459:—*

(a) na (b) Maagizo ya Kamati yamezingatiwa.

406. *Karadha za Binafsi na Masurufu—Aya ya 460:—*

(a) Kiasi cha Sh. 47,616/40 kimekusanywa, bado Sh. 199,498/25.

(b) Kiasi cha Sh. 170,531/50 kimekusanywa, bado Sh. 196,779/50. Ni matumaini ya Hazina kuwa kanuni ya urejeshaji masurufu pamoja na tozo ya asilimia 10 inatekelezwa.

407. *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka na Yenye Hati Pungufu—(Sh. 38,760,672/40)—Aya ya 461:—*

Kati ya hoja za Ukaguzi 117 za thamani ya Sh. 2,875,058/20 zilizosalia, hoja 73 za thamani ya Sh. 1,883,602/65 zimejibiwa na kufungwa, bado hoja 44 za thamani ya Sh. 991,455/55 ambazo zinaendelea kushughulikiwa.

408. *Shughuli Zisizo za Kawaida na/au Zenye Mashaka, Halmashauri ya Mji wa Tanga—(Sh. 100,000/-)—Aya ya 462:—*

(a) Hesabu ya Matumizi ya fedha hizo iliwasilishwa Ukaguzi.

409. *Matokeo ya Ukaguzi wa Ndani—Aya ya 463:—*

(a) Mkoa umeeleza kuwa vifaa vya thamani ya Sh. 68,793/65 vilikopeshwa kwa wafanyakazi ili kuwaongezea motisha, na fedha hizo zimekwisharejeshwa na wahusika. Ofisi iliyohusika na ukopeshaji vifaa hivyo imeagizwa kuacha mtindo huo kwa vile unakiuka kanuni za fedha.

(c) Hakuna Maagizo.

410. *Potevu za fedha na vifaa—Aya ya 464.:—*

(a) (i) Taarifa ya upotevu ilitayarishwa na kuwasilishwa Hazina. Na kati ya watumishi walioachiwa huru, moja alifariki, mwingine aliachishwa kazi, na watatu waliosalia Mkoa unakata kila mmoja Sh. 25,894/95 kufidia upotevu huo. Hadi wakati wa kuandika taarifa hii wote kwa pamoja wamekwisharejesha Sh. 21,724/95.

(ii) Hadi sasa mtuhumiwa huyo hajapatikana.

(b) (i) Taarifa ya upotevu iliwasilishwa Hazina.

(ii) Upelelezi wa Polisi bado unaendelea.

411. *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 465:—*

(a) (i) Vifaa vya thamani ya Sh. 2,000/- vimethibitika kupokelewa.

(ii) Vifaa vya thamani ya Sh. 1,000/- pia vimethibitika kupokelewa.

(b) (i) Hakuna maoni.

(iii) Vifaa vyote vya thamani ya Sh. 18,592/65 vimethibitika kupokelewa.

(c) Hakuna Maoni.

(d) (i)—(iv) Hakuna maoni.

(e) Vifaa vya thamani ya Sh. 600/- havijapatiwa maelezo.

(iii) Vifaa hivyo bado kutolewa maelezo.

(iv) Vifaa vyote vimethibitika kupokelewa.

(f) (i) Vifaa vya thamani ya Sh. 32,175/- vimethibitika kupokelewa na kuingizwa daftarini.

(ii) Vifaa vya thamani ya Sh. 22,920/- vimetolewa maelezo ya kuridhisha kuhusu matumizi yake.

(iv) Vifaa vya thamani ya Sh. 51,965/- vimetolewa maelezo ya kuridhisha kuhusu upokeaji na matumizi yake.

(v) Vifaa vyote vya thamani ya Sh 4,200/- vimethibitika kupokelewa.

(vi) Vifaa vya thamani ya Sh. 3,100/- vimetolewa maelezo ya kuridhisha. Vilivyosalia vinaendelea kutafutwa.

(vii) Vifaa vyote vya thamani ya Sh. 33,164/- vimepokelewa.

(viii) Mhusika anakatwa Sh. 3,100/- kufidia mifuko hiyo, na hadi sasa amekwishakatwa Sh. 2,800/-.

## FUNGU 87.—MKOA WA KAGERA

412. *Maswali ya Ukaguzi—Aya 466:—*

Kati ya maswali 192 yaliyokuwa yamesalia, maswali 34 yamejibiwa na kubakiza 158 ambayo yanaendelea kushughulikiwa.

413. *Matokeo ya Hesabu—Aya ya 467:—*

(a) na (b) Agizo la Kamati limezingatiwa.

414. *Usuluhisho wa hesabu ya Benki na Shahada ya Usahihi—Aya ya 468:—*

Usuluhisho wa hesabu hizo ulitayarishwa na kuwasilishwa Ukaguzi.

415. *Karadha za Binafsi, Masurufu na Karadha zingine—Aya ya 469:—*

(i) Kati ya kiasi cha Sh. 3,344,454/70 kilichokuwa hakijarejeshwa kuhusu karadha za binafsi, masurufu na karadha zingine, kiasi cha Sh. 1,886,403/95 kimerejeshwa na kubakiza Sh. 1,458,050/75. Mchanganuo wa marejesho hayo ni kama ifuatavyo:—

| *Aina ya Deni* | *Kiasi kilichorejeshwa* |
|---|---|
| (a) Karadha za binafsi ... ... ... | 54,620.00 |
| (b) Masurufu ... ... ... ... | 953,368.95 |
| (c) Karadha zingine ... ... ... | 878,415.00 |
| Jumla ... | 1,886,403.95 |

Juhudi ya kupata kiasi kilichosalia zinaendelea.

(ii) Kiasi cha Sh. 973,108/05 kimekwisharekebishwa, bado deni la Sh. 1,772,093/80 ambalo linashughulikiwa na Hazina.

416. *Mambo Yanayoathiri Hesabu za Jumla na Orodha Zake—Aya ya 470:—*

(i) Taarifa inayoonyesha kuwa hakuna malimbikizo yeyote yaliyokusanywa (NIL RETURN) iliwasilishwa Ukaguzi.

(ii) Suala la mfuko wa 'Plant and Transport Maintenance Fund' lingali likishughulikiwa na Wizara ya Ujenzi. Mpaka hapo ufumbuzi utakapopatikana Mkoa utapaswa kushughulikia hesabu za mfuko huo kulingana na mwongozo wa Hazina Na. 3 wa 1975.

(iii) Kazi ya kuitayarisha orodha hiyo upya inaendelea.

417. *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka—(Sh. 630,967/70) na Yenye Hati Pungufu—(Sh. 7,522,876/20)—Aya ya 471:—*

Kati ya kiasi cha Sh. 2,744,903.50 kilichosalia kuhusu matumizi hayo, kiasi cha Sh. 1,129,770/65 kimepatiwa maelezo ya kuridhisha. Juhudi ya kupata nyaraka zilizosalia zinaendelea.

418. *Ulegevu Katika Dhibiti ya Malipo ya Mishahara—Aya ya 472:—*

(i) Sh. 26,400/- zimekusanywa.

(ii) Sh. 4,800/- zimekusanywa.

(iii) Sh. 4,193/70 zimekusanywa.

(iv) Sh. 54,221/75 zimekusanywa.

Juhudi za ukusanyaji wa kiasi kilichosalia zinaendelea.

419. *Utovu wa Udhibiti wa Vifaa—Aya ya 473.:—*

(a)—(b) Maelezo kuhusu vipengere hivyo yaliwasilishwa Ukaguzi.

(c) Vifaa vya thamani ya Sh. 1,041/- bado kutolewa maelezo kuhusu upokeaji na matumizi yake.

(d) Hadi sasa fedha hizo hazijapatikana.

420. *Potevu ya Fedha na Vifaa—Aya ya 474:—*

(a) Mmoja wa watuhumiwa alirejesha Sh. 8,000/- kabla ya shitaka kufikishwa Mahakamani na hivyo kupunguza kiasi kilichopotea kuwa 104,320/-. Kesi bado inaendelea Mahakamani.

(b) Kesi bado inaendelea Mahakamani.

421. *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 475:—*

Kati ya taarifa 25 ambazo zilikuwa hazijajibiwa kwa miaka 1979/80 na 1980/81, taarifa 22 sasa zimekwishajibiwa na kubakiza taarifa 3 ambazo zinaendelea kushughulikiwa.

## FUNGU 88.—MKOA WA DAR ES SALAAM

422. *Taahira Kuletwa Hesabu za mwaka 1979/80—Aya ya 476:—*

(b) (i) Onyo la Kamati limezingatiwa. Mafanikio yatizamwe katika miaka ijayo.

(ii) Akaunti Na. 14.51 ilifunguliwa kwa ajili ya maduhuli.

(iii) Hakuna maoni zaidi.

(iv) Mkoa umeeleza kuwa baada ya kushauriana na Hazina utawasilisha hesabu za RDF kuanzia mwaka wa fedha 1983/84.

423. *Hesabu za Jumla na Orodha zake kwa mwaka 1980/81—Aya ya 477:—*

Hakuna maoni kuhusu aya hii.

424. *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 478:—*

Maswali 8 yamejibiwa na kufungwa kati ya maswali 11 yaliyokuwa yamesalia.

425. *Matumizi Yenye Nyaraka Pungufu—(Sh. 5,350,736/30)—Aya ya 479:—*

Nyaraka za thamani ya Sh. 18,738/30 zimepatikana, na nyaraka zilizosalia zinaendelea kutafutwa.

426. *Upotevu wa Fedha—Sh. 81,470/45—Aya ya 480:—*

Mtuhumiwa alikamatwa na kufikishwa Mahakamani, na kesi yake inaendelea.

427. *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 481.—*

Mkoa umezingatia agizo la Kamati.

## FUNGU 89.—MKOA WA RUKWA

428. *Kutowasilisha Majibu Sahihi Mkutanoni:—*

(a) na (b) Agizo la Kamati limetekelezwa.

429. *Maswali ya Ukaguzi—Aya ya 482:—*

Kati maswali 113 ya miaka tangu 1973/74 hadi 1980/81 maswali 12 tu yamejibiwa bado 101 ambayo Mkoa umesema unaendelea kuyashughulikia. Na kati ya zile taarifa maalum 13 zilizokuwa hazijajibiwa taarifa 3 zimejibiwa.

430. *Hesabu Hazikuletwa—Aya ya 483:*

Hazina haina maoni zaidi.

431. *Hali ya Uwekaji Hesabu na Shahada ya Usahihi—Aya ya 484:—*

(a) Agizo la Kamati limezingatiwa.

(b) Usuluhisho wa hesabu ya matumizi ya maendeleo umetayarishwa na kuwasilishwa Ukaguzi.

(c) na (d) Hazina haina maoni zaidi.

432. *Masurufu na Karadha—Aya ya 485:—*

(a) Michanganuo ya Karadha na Masurufu ilitayarishwa na wadaiwa wanaendelea kukatwa toka kwenye mishahara yao.

(b) Mchanganuo wa karadha zingine pia ulifanywa na wadaiwa wanandelea kulipa madeni yao.

(c) Kiasi cha Sh. 30,000/- kilimepwa kati ya kiasi cha Sh. 135,000/- kinachodaiwa.

433. *Matumizi Yasiyokuwa na Nyaraka na Yenye Hati Pungufu—(Sh. 1,521,707/80)—Aya ya 486:—*

Nyaraka zilizokuwa zinakosekana zimepatikana.

**434.** *Shughuli zenye Mashaka—Aya ya 487:—*

(a) (b) Mkoa haujatoa maelezo kuhusu vipengele hivyo.

**435.** *Orodha ya Mali na Dhima—Aya ya 488:—*

Orodha mpya zilitayarishwa na kuwasilishwa Ukaguzi.

**436.** *Ulegevu katika Dhibiti ya Ununuzi na Uwekaji Hesabu ya Vifaa—Aya ya 489:—*

(a) Vifaa vya thamani ya Sh. 611,674/25 vimethibitika kupokelewa na kuingizwa madaftarini.

**437.** *Potevu za Vifaa—(Sh. 102,901/00)—Aya ya 490:—*

(b) Taarifa ya potevu ya Sh. 9 800/- imetayarishwa na kutumwa Hazina.

(c) (d) Upelelezi wa Polisi bado unaendelea.

**438.** *Ukaguzi wa Mhakikimali—Aya ya 491:—*

Vipengele hivyo bado kutolewa maelezo ya kuridhisha.

## IV.—SERIKALI ZA MITAA

**439.—446.**

Hazina haina maoni kuhusu vifungu hivyo kwa vile hesabu za Serikali za mitaa hazipo chini ya usimamizi wake wa moja kwa moja kama ulivyo kwa Idara, Wizara na Mikoa. Kisheria Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa 'Proper Hesabu baada ya kukagua hesabu hizo hupaswa kutoa Taarifa yake kwa Officer' nakala kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri inayohusika ambaye huiwasilisha kwa Halmashauri hiyo ili ijadiliwe. Halmashauri hiyo baada ya kuijadili na kutoa mapendekezo yake ni wajibu wa Halmashauri yenyewe na Ofisi ya Waziri Mkuu kusimamia utekelezaji wa mapendekezo hayo. Hazina haihusiki.

## V.—MASUALA YA JUMLA

**447.**—*Hesabu za mwaka 1979/80—Kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati:—*

Maoni ya Hazina kuhusu taarifa hiyo yalitayarishwa na kuwasilishwa Bungeni.

**448.**—*Maswali ya Zamani ya ukaguzi Yasiyojibiwa:—*

Maagizo ya Kamati yamezingatiwa.

**449.**—Hakuna maoni.

Dar es Salaam
Septemba, 1984

G. Rutihinda
*Katibu Mkuu wa Hazina*